SUPA JACKPOT
TZS. 1,029,401,974
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Tume** ya Madini yatimuliwa katika nyumba za TBA

UKURASA 4


# Nipashe Jumapili

Jumapili Septemba 11, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581065

www.ippmedia.com

www.twitter.com/ni... www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Hatima ya Lukaku Inter kizungumkuti**

UKURASA 22




# Prof. Assad atia mkono sakata tozo

• **Apendekeza** wanaotumia magari ya kifahari serikalini watozwe... *Endelea ukurasa. 2*

UKURASA WA 3

## WAITWA KUPATA DOZI YA PILI YA UVIKO-19



WATU 269,000 ambao awali walipatiwa chanjo ya UVIKO-19 mkoani Shinyanga, hawakurudi kupata dozi ya pili, hivyo kusababisha...

UKURASA WA 5

## VIPODOZI VYA MILIONI 100/- VYATEKETEZWA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Ziwa limeteketeza tani tatu za vipodozi vyenye viambata vya sumu na bidhaa za chakula zilizoisha muda wa matumizi yake zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100.

## Tiba asili kutolewa hospitali za rufani



UKURASA 5



## Charles III Mfalme mpya wa Uingereza

UKURASA 17

MICHEZO SIMBA SC, YANGA ZATAKATA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikabidhiwa Tuzo Maalum na Kiongozi wa Madaktari Bingwa kutoka Jamhuri ya Watu wa China, Dr. Qu, alipofika Ikulu jijini Zanzibar jana, kwa ajili ya kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi katika Hospitali za Unguja na Pemba. **PICHA: IKULU**

# Prof. Assad atia neno sakata tozo

**Na Romana Mallya**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wa zamani, Prof. Mussa Assad, (pichani) amelizungumzia sakata la tozo za miamala ya kielektroniki ambazo utekelezaji wake umeanza katika mwaka huu mpya wa fedha.

Akizungumza katika kipindi cha Jahazi kinachorushwa na Kituo cha Redio cha Clouds juzi jioni, Prof. Assad alisema katika kufanya uamuzi wowote, kunakuwa na mambo mawili muhimu - moja kutazama faida ya jambo na pili, hasara zinazotokana na jambo husika.

"Unapoona faida inazidi hasara, unalitekeleza. Pale ambapo hasara zinazidi faida, unaliacha! Unapoona faida yenyewe siyo kubwa sana kulingana na hasara, linakuwa jambo lenye wasiwasi, unaweza kuliacha.

"Suala la tozo linaingia hapo, kwa kutazama kwa ujumla wake faida zake na hasara zake kwa serikali na wananchi. Ninaamini hasara zake ni kubwa kuliko faida. Ndiyo maana unaona Kamati Kuu ya CCM imeelekeza jambo hilo litazamwe upya, ili hizo faida na hasara zipimwe sawasawa wapate uamuzi utakaokuwa na faida kwa wananchi na serikali vilevile," alifafanua.



**VYANZO VIPYA**

Alipoulizwa mtazamo wake kuhusu vyanzo vipya vya mapato, Prof. Assad, msomi, mwenye weledi, ujuzi na uzoefu mkubwa wa uhasibu na udhibiti wa fedha mwenye Shahada ya Uzamivu wa Uhasibu (PhD in Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Southampton, Uingereza na Shahada ya Uzamivu katika Udhibiti wa Fedha (MA in Financial Accounting) kutoka Chuo Kikuu cha Dublin City, Jamhuri ya Ireland, alisema zipo mbinu nyingi za kupata fedha.

Alitolea mfano kuwamulika watu wanaotumia magari ya kifahari serikalini na mashirika yenye gharama kubwa, akiwa na ufafanuzi kwamba wanapaswa kutozwa kwa manufaa ya umma.

"Wanaotumia magari binafsi ofisini na wakitoka katika shughuli zao wanatumia magari hayo hayo, hao ndiyo wanaotakiwa kulipa kodi, inaitwa 'benefit in kind' faida ambayo si ya kifedha, kwa sababu wanapata faida hiyo, wanatakiwa kulipa.

"Mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi, wakuu wa mashirika ya umma, wote wanaotumia magari kama V8, VX, wote waingie katika kundi la kodi, tuwatoze kodi kwenye mishahara yao labda Sh. 150,000 kila mmoja zichangie.

"Yapo maeneo mengi ambayo tunaweza kuyaainisha na kupata kodi kwa wingi, lakini si hivyo tu, kodi inatakiwa iwe fundisho kuhakikisha tabia fulani fulani haziendelezwi. Kama ananunua gari, basi liwe la gharama ya chini kidogo na sisi wananchi tupate faida," alishauri.

Prof. Assad alishika nafasi ya CAG kuanzia Desemba Mosi, 2014, alipoteuliwa na Rais wa wakati huo, Jakaya Kikwete, hadi Novemba 3, 2019 Rais John Magufuli alipomteua Charles Kichere kushika nafasi hiyo, akiwa ni CAG wa saba tangu nchi ipate uhuru.

Kabla ya uteuzi huo, Prof. Assad alikuwa Profesa Mshiriki Idara ya Uhasibu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na alichukua nafasi ya Ludovick Utouh, ambaye alistaafu kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma.

Siku tatu zilizopita, Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, ikiwa ni siku moja baada ya Kamati Kuu ya CCM kuketi, alisema kikao hicho kimetoa maelekezo sita kwa serikali ikiwamo kutazama hali halisi na kuchukua hatua stahiki kuhusu utozaji wake wa kodi.

Shaka alisema hatua ambazo chama hicho kimetaka zichukuliwe ni pamoja na kuzingatia maoni na ushauri wa wananchi.

Muda mfupi baada ya kuanza utekelezaji wa tozo hizo za kielektroniki katika mwaka huu wa fedha, wadau mbalimbali kwa nyakati tofauti, wamekuwa wakijitokeza kuzipinga huku wakitoa mapendekezo yao kuhusu hatua mbadala za kuchukua kuiwezesha serikali kupata mapato.

## Rais Samia atangaza siku tano maombolezo kifo cha Malkia Elizabeth

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametangaza siku tano za maombolezo kitaifa kuanzia jana kutokana na kifo cha Malkia wa Uingereza, Elizabeth II kilichotokea Alhamisi huko Scotland.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, maombolezo hayo yalianza jana.

"Katika kipindi chote cha maombolezo, bendera zote zitapepea nusu mlingoti nchini Tanzania zikiwamo kwenye balozi zetu," ilibainisha taarifa hiyo ya Ikulu.

Rais Samia pia amewaomba Watanzania wote kuungana na Waingereza katika kipindi hicho cha kuondokewa na kiongozi wao.

Kwa mujibu wa DW Swahili, Mfalme Charles III wa Uingereza ambaye ndiye mrithi wa nafasi hiyo, amehutubia taifa lake kwa mara ya kwanza tangu kutokea kifo cha mama yake Malkia Elizabeth II.

Katika hotuba yake aliyoitoa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Paulo, tangu awe Mfalme, alimtaja Malkia Elizabeth II kuwa ni mtu wa mfano kwake na familia yao kwa ujumla.

Kutokana na yale yote aliyoyatenda mama yake, Mfalme amesema wana deni lake la dhati kwa kutimiza upendo na mwongozo.

Mfalme Charles III ameonyesha nia ya dhati kwa kuanza majukumu yake kwa kuendeleza huduma ya maisha yote ya mfano wa Malkia Elizabeth II, kwa kuzingatia hali ya sasa, chini ya enzi mpya.

Katika hotuba ya dakika tisa na nusu ambayo ilirekodiwa awali, akiwa na picha ya Malkia mbele yake, alitoa ahadi ya kuwahudumia Waingereza kwa maisha yake yote, kuanzia sasa.

Mfalme huyo alisema kama ilivyokuwa kwa Malkia mwenyewe alivyofanya majukumu yake kwa ibada isiyoyumba, naye pia anajitolea kwa dhati katika muda wote uliosalia ambao Mungu atamjalia kwa kuzingatia kanuni za kikatiba katika moyo wa taifa lao.

Hotuba ya mfalme ilitangazwa kwenye televisheni na mitandaoni kutoka katika Kanisa kubwa la Mtakatifu Paulo ambako watu wapatao 2,000 walihudhuria ibada hiyo ya ukumbusho kwa Malkia.

Ibada hiyo pia ilihudhuriwa na Waziri Mkuu mpya wa Uingereza Liz Truss na maofisa katika serikali yake pamoja na mamia ya watu.

Kwenye ukurasa wake rasmi wa Twitter, mfanyabiashara maarufu nchini, Mohammed Dewji 'Mo', aliandika jana: "Ningependa kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia ya kifalme, raia wa Uingereza na Jumuiya ya Madola kwa kuondokewa na Malkia Elizabeth II, aliyetawala kwa muda mrefu zaidi Uingereza.

"Wakati wa miongo saba ya utawala wake, Malkia aliongoza kwa nguvu, utulivu na umoja. Pumzika kwa amani Malkia."

## HABARI KITAIFA



Wafanyabiashara waliokuwa wakifanya shughuli zao kwenye eneo la mwekezaji, Temeke Vetenari, mkoani Dar es Salaam, wakihamisha bidhaa zao jana, kupisha kuvunjwa kwa vibanda vyao ili kupisha ujenzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madiwani wacharuka tembo kuua wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MADIWANI wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida wameijia juu Idara ya Mazingira na Maliasili, wakiitaka ichukue hatua za haraka kudhibiti tembo ambao wamekuwa wakiua na kujeruhi watu katika matukio yanayojitokeza mara kwa mara ndani ya halmashauri hiyo.

Walipaza kilio hicho juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Itigi kufuatia kutolewa taarifa za tembo kuua wanawake wawili na kujeruhi mmoja katika tukio lililotokea hivi karibuni Kata ya Mgandu wilayani humo.

Diwani wa Mgandu, Martin Kapona, alisema wanawake hao waliuawa kwa kukanyangwa na tembo na kupoteza maisha papo hapo wakati wakiwa shambani na aliyejeruhiwa, sasa anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Mtakatifu Gaspar, Itigi.

"Majeruhi aliyejeruhiwa tangu alazwe hospitalini, Idara ya Mazingira na Maliasili haijatoa ushirikiano wowote na familia ya majeruhi huyo inateseka kwa kumuuguza," alilalamika.

Kapona alisema tembo wamekuwa kero kubwa Itigi kwa kuwa wamekuwa wakivamia mashamba ya wananchi, kuua na kujeruhi wananchi lakini Idara ya Mazingira na Maliasili haionekani kutoa ushirikiano wowote.

"Idara ya Mazingira na Maliasili kama inawezekana itoe kifuta jasho kwa waliofiwa na ndugu zao na majeruhi alipwe gharama za matibabu anazotumia maana kama mwananchi angeua tembo, hivi sasa angekuwa jela, lakini tembo ameua na kujeruhi mwananchi, nguvu kazi imepungua, mama anashinda amelala kitandani," alililalamika zaidi diwani huyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba, alikiri maeneo mengi ya Itigi yameathiriwa na tembo ambao wanavamia wananchi na kuharibu mazao mashambani.

Simba alisema tatizo lililopo ni kwamba Idara ya Mazingira na Maliasili ina mtumishi mmoja, hivyo inakuwa vigumu kufika kila kijiji kuangalia namna ya kutatua matatizo ya wanyamapori hao vijijini.

Alitoa wito kwa watumishi kushirikiana ili kukabiliana na tatizo hilo la tembo kwa kuwa linawakosesha amani wananchi, husasani wa vijijini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itigi, John Mgalula, alisema kuwa baada ya tukio hilo kutokea, alikwenda kijijini huko na kushuhudia tatizo hilo.

Alisema tatizo lingine ni kwamba baadhi ya wananchi wanapowaona tembo, wamekuwa wakidiriki kutaka kupambana nao, hivyo akashauri madiwani na watumishi wasaidie kuelimisha wananchi ili wanapowaona wanyama hao watoe taarifa kwa mamlaka husika badala ya kujaribu kupambana nao.

# Waitwa kupata dozi ya pili ya UVIKO-19

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATU 269,000 ambao awali walipatiwa chanjo ya UVIKO-19 mkoani Shinyanga, hawakurudi kupata dozi ya pili, hivyo kusababisha miili yao kutokuwa na kinga imara kukabiliana na virusi vya corona.

Chanjo ya UVIKO-19 ambayo inatolewa kwa dozi mbili ni ya Sinopharm, Pfizer na Moderna.

Mratibu wa Chanjo mkoani Shinyanga, Timothy Sosoma, alibainisha hayo juzi alipozungumza na Nipashe na kutoa wito kwa watu hao ambao hawakurudi kupata dozi ya pili, wakaipate dozi hiyo ili waimarishe kinga zao.

"Mkoa wa Shinyanga tulikuwa na lengo la kuchanja watu 1,011,085 chanjo ya UVIKO-19, hadi kufikia Agosti 31 mwaka huu, watu waliopata dozi kamili ni 735,844, sawa na asilimia 73 na kuufanya mkoa kushika nafasi ya tano kitaifa kwa utoaji wa chanjo.

"Watu ambao hawajakamilisha dozi ya pili ya chanjo ya UVIKO-19 ni 269,000 ambao walipatiwa chanjo ya Sinopharm, Pfizer na Moderna na tuliwachanja katika mazingira mbalimbali ikiwamo kwenye minada. Tunawashauri warudi kupata dozi ya pili ili kinga zao ziwe imara zaidi," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, alisema mtu ambaye hajakamilisha dozi ya pili chanjo ya UVIKO-19, hawezi kupata madhara yoyote kiafya, lakini akipata maambukizi ya corona, dozi hiyo moja haiwezi kumsaidia kwa kuwa haitakuwa na nguvu hadi akamilishe dozi mbili.

Alifafanua kuwa mtu akishapata dozi moja ya chanjo ya UVIKO-19, anapaswa asichelewe kupata dozi ya pili ndani ya siku 90 na endapo akipitisha siku hizo, haina shida lakini siku akipata dozi ya pili atakuwa imeiamsha ile ya kwanza na kuimarisha kinga yake.

Alisema mtu mwenye dozi moja ya chanjo, hana tofauti na yule ambaye hakupata chanjo kabisa na siku akipata maambukizi ya corona, madhara yake yatakuwa pale pale.

"Yule aliyepata dozi kamili, hawezi kupata madhara makubwa, bali atakuwa salama. Ninatoa wito kwa wananchi wajitokeze kupata chanjo ya UVIKO-19 na kukamilisha dozi," alishauri.


## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**SUBILA SAID MKALI** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **TVS** yenye usajili namba **MC 361 CHB**, CHASSIS NAMBA: **MD6M14PA7K4E11777** na ENGINE NAMBA: **AK4EK4711592.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **KW/RB/4010/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**THOMAS D.C MALIMA** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma: cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.078/052** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MUGANGO SECONDARY** SCHOOL mwaka 2001 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0370/572** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **IFAKARA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2004. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB 358587/2022**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA SONGEA ILIYOPO SONGEA**

**RUFAA YA JINAI NA. 12 YA MWAKA 2022**

**CHRISTIAN KAYOMBO ......................MWOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**TAMU KISINZA NDUGULILE......................MJIBU RUFAA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA:-**
**TAMU KISINZA NDUGULILE**
**POPOTE ULIPO**

Hii ni kukutaarifu kwamba Rufaa ya jinai tajwa hapo juu imepangwa kusikilizwa tarehe 13 mwezi septemba mwaka 2022 saa 3.00 asubuhi mbele ya Mh. A.C JEMBE Hakimu mkazi wa wilaya ya Songea. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hutahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hilo la rufaa litasikilizwa bila wewe kuwepo

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 18 mwezi 8 mwaka 2022

HAKIMU MKAZI WA WILAYA YA SONGEA

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HASHIRY KASIM MABOTE** antangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC **301 CEH**, **CHASSIS NAMBA: KFKNPGA0000003** na ENGINE NAMBA: **162 FMJNPN00003.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/358229/2022**

TRUST RECOVERIES LTD

JUAKALI STREET, MWANJELWA P.O. BOX 462 MBEYA, TANZANIA
TEL/FAX: 0765 387 832, 0742 674 672, EMAIL: trustrecoverieslimited@gmail.com

## NOTISI / TANGAZO/TAARIFA

**TRUST RECOVERIES LIMITED** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **LETSHEGO BANK (T) LIMITED,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, na endapo mdaiwa atashindwa kulipa mkopo wake, tutafanya mnada wa hadhara kuuza dhamana kama ratiba inavyoonyesha.

| NA | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE/MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AUGUSTINO KOMBA | MBEYA | AUGUSTINO KOMBA | Plot no. 844 BLOCK HH MBYLR | ISYESYE, MBEYA | 28/09/2022, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

1170407O2

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
3. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI; Tupigie simu no. 0742 674 672 au 0678 799 566.**

# Tume Madini yatimuliwa kwenye nyumba za TBA

**Na Richard Makore,** MWANZA

TUME ya Madini Kanda ya Ziwa imefukuzwa upangaji kwenye nyumba za Wakala wa Majengo (TBA) kutokana na kushindwa kulipa kodi ya pango kwa zaidi ya miaka minne.

Jijini Mwanza juzi, Kaimu Meneja wa TBA, Moses Urio, alitangaza kuchukuliwa kwa uamuzi huo alipozungumza na waandishi wa habari katika operesheni maalum ya kuwaondoa wadaiwa sugu katika nyumba zao.

Alisema tume hiyo ni miongoni mwa wadaiwa sugu wanaodaiwa Sh. milioni 200 na kwamba operesheni hiyo inawalenga wote walioshindwa kulipa kodi katika nyumba hizo. Urio alisema operesheni hiyo inalenga kuwafikia na kuwaondoa wadaiwa wote sugu mkoani Mwanza waliopanga katika nyumba za TBA.

Alisema kazi hiyo inafanywa na Kampuni ya Udalali ya Twins Auctions, ikitarajiwa kukamilika ndani ya siku tatu.

Wapangaji hao ni walioko katika nyumba za wakala huo zilizoko maeneo mbalimbali mkoani Mwanza na walishindwa kulipa kodi licha ya kupewa muda wa wiki mbili kufanya hivyo.

Urio aliongeza kuwa baadhi ya wapangaji walikimbia nyumba hizo baada ya kusikia kuna operesheni hiyo, akifafanua kuwa walifunga milango.




Wafanyabiashara wadogo 'Machinga', wakiendelea na biashara zao katika eneo la Kimara Mwisho, mkoani Dar es Salaam juzi, licha ya kuwapo kwa tangazo la zuio lililowekwa na Manispaa ya Ubungo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mbaroni tuhuma kuvunja nyumba usiku na kupora

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watu 10 wanaotuhumiwa kuvunja nyumba za wananchi wa Kinyerezi Kibaga jijini Dar es Salaam na kupora mali mbalimbali.

Usiku wa kuamkia Septemba 6 mwaka huu, kundi la vijana takriban 30 wahalifu wa mitaani, maarufu panya road lilivamia nyumba 15 na kujeruhi watu wanne na kupora fedha na mali katika mtaa huo tajwa.

Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, Wiliam Mkonda, alisema juzi kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na operesheni ya kuzuia uhalifu maeneo mbalimbali.

Alisema kutokana na tukio hilo lililotokea saa 3:13 usiku wa siku hiyo, Jeshi la Polisi lilimkamata Selemani Kalembo (57), maarufu Sele Bonge, mkazi wa Vingunguti na wenzake tisa, wakiwa na gari lenye namba za usajili T 218 BYS aina ya Noah.

Alisema kuwa watu hao walikutwa wakiwa na vifaa mbalimbali vya kuvunjia, televisheni nne, kamba na mfuko wa kufichia viambaza (TV) baada ya kuiba.

"Mahojiano ya kina yanaendelea ili kuwakamata wote walioshirikiana nao. Jeshi la Polisi limeendelea na vikao na wananchi wa Kinyerezi na maeneo mengine ya jiji, vyenye lengo la kuimarisha na kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi, kwa maeneo ambayo hayana," alisema.

Kamanda Mkonda aliwataka viongozi wa serikali za mitaa na wananchi kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi katika mikakati ya kupeana elimu na kuhakikisha kila mtaa unakuwa navyo.

"Tunawaomba wananchi waendelee kushirikiana na polisi katika kutoa taarifa za kuwabaini wahalifu na linaahidi kutunza siri hizo.

"Tunaendelea na operesheni maalum maeneo yote na tunatoa onyo kwa mtu au kikundi kinachojihusisha na vitendo vya kihalifu kuacha mara moja," alisema.

## Madereva wasafirishaji kemikali waonywa

**Na Mary Geofrey**

MADEREVA wanaosafirisha kemikali hatarishi, wametahadharishwa kutokutumia dawa za kulevya pindi wanapokuwa safarini ili kuepuka ajali.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Uchunguzi wa Bidhaa na Mazingira kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Sabanitho Mtega, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili kwa madereva wanaosafirisha kemikali kutoka Kampuni ya Golden Coach ya Dar es Salaam.

"Kutokana na vijana kuwa nguvu kazi ya taifa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imeona umuhimu wa kuandaa mafunzo haya kwa madereva wanaosafirisha kemikali hatarishi.

"Niwasisitize madereva wote nchini wanaosafirisha kemikali hatarishi, kuepuka kuendesha chombo cha moto ukiwa umetumia kilevi kwa sababu ni hatari katika taaluma yako, mzigo uliobeba na mazingira unayopita na mzigo huo wa kemikali," alisema.

Mtega aliongeza kuwa matumizi ya dawa za kulevya wakati wa usafirishaji huathiri uwezo wa kufikiri, kutafakari na kuona na matokeo yake dereva kushindwa kuchukua tahadhari za haraka.

Alisema ajali zinazotokana na madereva waliotumia vilevi husababisha hasara za mali, mazingira na maisha ya dereva husika na watu waliopo karibu na eneo la ajali.

Mtega alitoa rai kwa wamiliki wa kampuni za kusafirisha kemikali hatarishi, kuendelea kutoa elimu kwa madereva wao kuhusu ufahamu wa makundi ya kemikali wanazosafirisha kwa kushirikiana na GCLA.

Mmoja wa madereva hao, Saidi Kisindula, alisema baada ya kupata mafunzo ya usafirishaji salama wa kemikali kutoka GCLA, atachukua tahadhari anaposafirisha mizigo ya kemikali na kuahidi kuwa atatoa elimu kwa madereva wenzake namna ya kuepuka matumizi ya dawa za kulevya na kujikinga na kemikali wanazosafirisha kama vile sulphur, ammonium na zingine.

HABARI KITAIFA

# Moto ulivyoteketeza bweni shuleni mkoani Mara

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

WANAFUNZI 46 wa Shule ya Sekondari Mara wilayani Musoma mkoani Mara wamepoteza mali zao baada ya bweni lao kuteketea kwa moto.

Tukio hilo lilitokea juzi, moto huo ukiteketeza vitu mbalimbali vya wanafunzi hao, vikiwamo vitanda, magodoro, masanduku, nguo za shule na madaftari.

Baadhi ya wanafunzi, wakizungumzia tukio hilo, walisema moto huo ulizuka ghafla na kuwaka kwa kasi majira ya saa tano asubuhi wakati wao wakiwa darasani wakiendelea na masomo.

Walisema baada ya kuona moto huo ukiwaka, walijaribu kuuzima kwa kutumia mchanga, lakini uliwazidi nguvu na kuteketeza jengo lote na vitu vyote vilivyokuwapo ndani.

Akizungumza na wanafunzi na walimu wa shule hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Khalfan Haule, aliwataka wawe watulivu katika kipindi hiki kigumu kwao.

Haule pia aliliagiza Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilayani Musoma mkoani Mara kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto huo.

Alisema uchunguzi huo pia utabaini njia bora kwa uongozi wa shule kufanya ukarabati wa jengo hilo.

"Ninaomba mtu yeyote mwenye taarifa za siri kuhusu chanzo cha moto huu, amfikishie mwalimu yeyote ama mfanyakazi ywyote wa shule hii," aliagiza.

Alisema kwa sasa wanafunzi hao watahamishiwa kwa muda katika chumba cha kompyuta shuleni huko, huku akiahidi kuwatafutia magodoro na madaftari, akihimiza wanafunzi wenzao kuwasaidia nguo.

# Vipodozi vya milioni 100/- vyateketezwa

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Ziwa limeteketeza tani tatu za vipodozi vyenye viambata vya sumu na bidhaa za chakula zilizoisha muda wa matumizi yake zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100.

Wakati wa uteketezaji wa bidhaa hizo juzi, Ofisa Mdhibiti Ubora wa TBS Kanda ya Ziwa, Arnold Kubigwa, alisema zilikamatwa sokoni wakati wa ukaguzi wao.

Alisema wananchi wanapaswa kukagua bidhaa mbalimbali wanazonunua ili kuona viambata vyake na muda wa kutengenezwa, pia kujua matumizi ili kuepuka madhara ya kiafya. Kubigwa pia aliwataka wafanyabiashara kuwa waaminifu katika kuuza, kuhifadhi na kuondoa bidhaa zilizoisha muda wake kwa mujibu wa sheria. "Kama watashindwa kuondoa bidhaa hizo, sisi kama shirika tutaziondoa na tutachukua hatua kali za kisheria dhidi yao," Kubigwa alionya.

Baadhi ya wananchi mkoani Mwanza wameomba serikali kuongeza ukaguzi ili kuondoa mwanya wa baadhi ya wafanyabiashara kuuza bidhaa zisizo salama na kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

"Sheria ifuate mkondo wake, haiwezekani kitu kimeisha muda wake halafu unamuuzia binadamu mwenzako, huu ni ukatili na kukosa utu," alikemea Happiness Enock, mkazi wa jijini Mwanza.

Julius John, mkazi mwingine wa jijini, alisema wafanyabiashara wengi wanaangalia faida na wapo tayari kuuza vitu visivyofaa kwa matumizi, cha maana kwao ni waingize fedha na siyo kuangalia afya za watu.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akizungumza na wakuu wa vyombo vya usalama vya wizara yake, katika kikao kazi, jijini Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Christopher Kadio. **PICHA: WMNN**

# Tiba asili kutolewa hospitali za rufani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI iko mbioni kuanza kutoa huduma jumuishi za tiba asili na tiba za kisasa kwenye baadhi ya hospitali zake zikiwamo za rufani ili kufanya majaribio ya huduma hizo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika yaliyofanyika mkoani Morogoro.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kusirye Ukio, waziri huyo alisema tayari serikali imeanza utoaji wa huduma hizo katika vituo vya Momela, Wilaya ya Meru mkoani Arusha na Maibong-SukiDar, Magomeni mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuanzishwa kwa huduma hizo ni mafanikio makubwa tangu uhuru kwa kuwa nchi imefanya kazi kubwa kuboresha na kuendeleza huduma za tiba asili.

Aliyataja mafanikio hayo ni pamoja na tiba asili kutambuliwa katika sera ya afya, kutungwa kwa sheria ya tiba asili na tiba mbadala, kanuni na miongozo mbalimbali pamoja na kuongezeka kwa utafiti wa tiba asili unaofanywa na vyuo vikuu vya serikali.

Mengine ni ujenzi wa kiwanda cha kuchakata dawa za asili cha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) huko Mabibo mkoani Dar es Salaam.

Pia utoaji huduma jumuishi za tiba asili na tiba za kisasa katika vituo vya Momela Wilaya ya Meru mkoani Arusha na Maibong-SukiDar, Magomeni mkoani Dar es Salaam.

Waziri Ummy alisema mchango wa tiba asili umedhihirika zaidi wakati wa mapambano ya UVIKO-19 na viongozi na serikali za kiafrika zinawajibika kuona umuhimu wa kuboresha tiba hiyo katika mapambano ya adui maradhi. "Hizi huduma za tiba asili zilitumika sana wakati wa Covid-19 na zileta tija kubwa sana kuwahudumia wahitaji ambapo dawa takriban 21 za asili zilitumika. Watanzania wamekuwa na imani kubwa na huduma za tiba asili," alisema.

Waziri Ummy, kupitia hutoba yake hiyo, alisema kuendeleza huduma za tiba asili nchini ni moja ya vipaumbele vya serikali na hata Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo kwayo serikali itapimwa. Aliwataka waganga wa tiba asili na tiba mbadala kutengeneza dawa zenye ubora na kuhakikiwa na mamlaka zinazotambulika ikiwa pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu usalama wa dawa zao.

Waziri huyo aliwaonya waganga kuchanganya dawa za kisasa kwenye dawa zinazotengenezwa na kuuzwa kwa wahitaji na kuongeza kuwa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na vyuo inaendelea kufuatilia dawa zote za tiba asili zilizoko sokoni.

Alisema dawa yoyote itakayokutwa imechanganywa na dawa za kisasa, hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mmiliki wa dawa husika.

Mkurugenzi Msaidizi wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kutoka Wizara ya Afya, Dk. Paulo Mhame, aliwakumbusha waganga hao kuzingatia miiko na maadili ili kujiepusha kuchukuliwa hatua za kisheria wanapokwenda kinyume.

Alilipongeza Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kuendelea kusajili waganga hao katika vituo vya kutolea huduma za afya katika mikoa yao.

Dk. Mhame alisema katika maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika ya 2022 yaliyofanyika mkoani Morogoro, zaidi ya waganga 500 kutoka maeneo mbalimbali nchini walikwenda Morogoro kusajiliwa papo hapo na kupata vyeti vyao.

Mkurugenzi wa Uzamili na Utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA ), Prof. Esron Karimuribo, alisema Tanzania ina mazao mazuri yanayofanya vizuri, yamethibitishwa ubora katika tiba na kuhakikiwa yanafanya vizuri.

Alisema chuo kikuu hicho kinaendelea kutoa elimu kwa wataalamu wa tiba asili na wameanza na utaalamu wa vifungashio kwa dawa hizo na utoaji wa dozi kamili ili kupata matokeo mazuri.

Mapema Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Elizabeth Lema, alisema wataendelea kuwakamata vishoka na matapeli wanaopita kuwasajili waganga hao na hatua kali za kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la CCM kwa serikali tozo za miamala litekelezwe

**KATIKA** siku za karibuni kumekuwa na kilio kutoka kwa wananchi kuhusu tozo za miamala ya kielektroniki kwamba zimekuwa mzigo kwao na kusababisha hali ya maisha kuwa ngumu zaidi.

Kwa mujibu wa malalamiko ya wananchi hao, wanapotuma fedha kwa njia ya simu wanakatwa kiasi kikubwa na pia wanapotoa fedha vivyo hivyo. Hata katika miamala ya kibenki tozo zimekuwa juu hatua ambayo imezua mijadala mingi kupitia mitandao ya kijamii pamoja na wadau mbalimbali wakiwamo wasomi.

Aidha, kutokana na mzigo wa tozo hizo, baadhi ya kampuni za simu za mkononi zimepaza sauti juu ya hasara zinazopata za mabilioni ya shilingi. Sababu kubwa inayotolewa ni kupungua kwa wateja wanaotumia miamala ya fedha kwa njia ya simu pamoja na matumizi ya vifurushi.

Wakati baadhi ya kampuni za simu zimelalamikia hasara, haijawekwa bayana kama kuna athari kwa upande wa benki kwa sababu hakuna taarifa rasmi zilizotolewa. Hata hivyo, kutokana na hali halisi, inawezekana kuna mtikisiko kwa sababu ya watu kuacha kutumia huduma za kibenki.

Licha ya kulalamika kukumbana na mzigo wa tozo, wananchi na wadau hao wametaka serikali kuchukua hatua ili kuwapunguzia adha na kuwafanya wafurahie huduma mbalimbali zinazotokana na miamala ya benki na simu za mkononi.

Kuendelea kuwapo kwa malalamiko ya tozo, mapema wiki hii mawaziri wa fedha, sera bunge na uratibu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) waliibuka na kutoa ufafanuzi ambao kwa kiasi kikubwa uliamsha hasira kutoka kwa wananchi na wadau hata viongozi hao kukejeliwa kuwa wanajibu kwa jeuri kwa sababu wameshiba!

Hata hivyo, Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kikao chake cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) kilichofanyika Jumatano jijini Dar es Salaam, kiliingilia kati na kuiagiza serikali kuchukua hatua dhidi ya kilio hicho cha wananchi, kubwa zaidi ikitakiwa kusikiliza maoni ya wananchi.

Katika taarifa yake, CCM iliweka bayana kwamba serikali ni sikivu hivyo ina imani kilio hicho cha wananchi kitasikilizwa na hatimaye kuwatua wananchi mzigo huo wa tozo za miamala ya simu na benki.


Pamoja na agizo hilo, ni vyema viongozi waliopewa dhamana katika nafasi mbalimbali, wakaacha ubabe na kutoa majibu ambayo yanawakwaza wananchi na hata kuifanya serikali kulaumiwa. Mfano ni kauli za mawaziri waliokuja wakijibu hoja kuhusu tozo ambapo mmoja alitoa maneno ya kuudhi na hata kuwafanya wananchi kupitia mitandao ya kijamii kumshambulia na kumwelezea kuwa amelewa madaraka.

Viongozi hao wanapaswa kutambua kuwa vyeo walivyo navyo ni dhamana, hivyo wanapaswa kuwatumikia wananchi badala ya kujiona ni mabwana na wananchi ni watwana, na hatimaye tukarejea enzi za ukoloni na kuibuka vitendo vya kidikteta.

Jambo la muhimu ni kwamba serikali, kama CCM ilivyoagiza, ifanye kila liwezekanalo kuhakikisha wananchi wanapunguziwa makali ya tozo kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Matumizi ya Fedha iliyopitishwa katika Bunge la Bajeti. Pia serikali inatakiwa kubuni vyanzo vya mapato ambavyo si vya kuwaumiza wananchi kama ilivyo kwenye tozo za miamala.

Ni matumaini kwamba serikali itachukua hatua madhubuti na kwa kuwa Bunge linaanza mkutano wake keshokutwa, muswada wa mabadiliko ya sheria ya fedha pamoja na mambo mengine utajielekeza kwenye tozo zinazolalamikiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Huduma jumuishi za tiba asili na kisasa zingepanuliwa zaidi

Na Sabato Kasika

**HUDUMA** ya tiba asili inatajwa kuwa na mchango mkubwa katika matibabu mbalimbali, ambapo imekuwa ikionyesha matokeo mazuri hali inayowafanya watu kuendelea kuiamini na kuipa uzito.

Kutokana na ukweli huo, serikali imeanza utoaji wa huduma jumuishi ya tiba asili na tiba ya kisasa katika baadhi ya vituo vya afya, kwa kuwa mchango wa tiba hizo umejidhihirisha wakati wa mapambano ya UVIKO-19.

Lakini pia ninashauri viongozi na serikali za Kiafrika kuwajibika kuona umuhimu wa kuboresha tiba hiyo katika mapambano ya adui maradhi kwa lengo la kulinda afya za wananchi wao.

Ni hivi karubuni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Dk. Kusirye Ukio alisema hayo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika mjini Morogoro, akimwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Katika maelezo yake, akabainisha kuwa huduma hiyo imeanza kutolewa katika vituo vya afya vya Momela Wilaya ya Meru na Maibong-Suki mkoani Arusha na Magomeni jijini Dar es Salaam.

Serikali inakiri kwamba mchango wa tiba asili umedhihirika zaidi wakati wa mapambano ya UVIKO-19, ni wazi sasa ipo haja ya kupanua huduma jumuishi ya tiba za asili na za kisasa ili Watanzania wengi zaidi waipate.

Ninaamini kwamba, kuanzishwa kwa huduma hizo kunaweza kuwa ni mafanikio makubwa hasa kwa kuzingatia kwamba tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961 kulikuwa hakujakuwapo huduma kama hiyo.

Inaelezwa kuwa tiba asili zinatambuliwa katika Sera ya Afya, huku kukiwa kumetungwa Sheria ya Tiba Asili/Mbadala, kanuni na miongozo mbalimbali na kuongezeka kwa tafiti za tiba asili zinazofanywa na vyuo vikuu vya serikali.

Dk. Ukio kwa niaba ya Waziri Ummy anakiri kuwa wakati wa UVIKO-19 huduma za tiba asili zilifanya kazi ya kuwahudumia wahitaji kwa kutumia dawa takribani 21, ni vyema kasi ya kupanua huduma jumuishi ikaongezeka.

Lakini pia kwa kuwa serikali inasema suala la kuendeleza huduma za tiba asili ni mojawapo ya kipaumbele, basi waganga wa tiba hizo wangejitahidi kutengeneza dawa zenye ubora.

Hatua hiyo itasaidia kuhakikiwa na mamlaka zinazotambulika ikiwa ni pamoja na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhusu usalama wa dawa zao, kwani zile zinazothibitishwa kutokuwa na usalama kwa kiwango kinachokubalika ndizo zisajiliwe kwenye Baraza la Tiba Asilia.

Pamoja na hayo, kuna onyo la serikali la kuwataka wanganga wa tiba asili kuacha kuchanganya dawa za kisasa kwenye dawa zinazotengenezwa na kuuzwa kwa wahitaji, kwa kuwa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na vyuo inaendelea kufuatilia dawa zote za tiba asili zilizopo sokoni.

Ili kufanikisha huduma hiyo katika jamii, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, vinatakiwa kuacha matangazo yasiyo na vibali kutoka Baraza la Tiba Asili/Mbadala, badala yake elimu zaidi itumike kuelimisha Watanzania.

Nadhani kwa njia hiyo, waganga ambao wamekuwa wakijitangaza kutibu maradhi mbalimbali bila vibali wanaweza kukosa nguvu na hatimaye kujiondoa kwenye shughuli hiyo.

Ingekuwa vyema pia iwapo suala la waganga wote wa tiba asili kujisajili katika baraza hilo ili kazi zao zitambulike na kuingizwa katika huduma jumuishi ili Watanzania zaidi kunufaika na huduma hiyo.

Ninaamini kuwa karne hii ya sayansi na teknolojia si ya kufanya shughuli za tiba ya asili kiujanja ujanja tu, bali ingefaa dawa zao zikadhibitishwa ili kusaidia katika matibabu kama ilivyokuwa wakati wa mlipuko wa UVIKO-19.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Sababu kifo EAC ya kwanza na mtikisiko wa jumuiya mpya



Na Pascal Mayalla

SAFU hii ya 'Kwa Maslahi ya Taifa', leo inaendelea na sehemu ya pili ya Ijue Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Fursa za Mtangamano.

Wiki iliyopita nilianza kwa kuitambulisha EAC na kusema ni jumuiya ya pili baada ya ile ya kwanza kuvunjika mwaka 1977.

Katika mwendelezo wa mada hii, Leo tunaanzia historia ya sababu ya jumuiya ya mwanzo kuvunjika ili kuzuia sababu hizo zisije kusababisha na jumuiya hii ya pili kuvunjika.

Kuvunjika kwa jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki, kulitokana na sababu nyingi lakini kubwa ya kwanza ni tofauti za kisiasa, kiitikadi na mifumo ya uchumi baina ya nchi wanachama. Tanzania tulifuata siasa ya Ujamaa na Kujitegemea wakati Kenya iliendelea na mfumo wa uchumi wa kibepari na soko huria iliourithi kutoka katika uchumi wa kikoloni.

Uganda ilitawaliwa kidikteta na Nduli Idi Amini Dada, hivyo kutaifisha kila kitu kuwa mali ya umma.

Sababu zingine zilizochangia kuvunjika ni pamoja na ukosefu wa utashi wa kisiasa (political will) baina ya viongozi wakuu wa nchi wanachama kwa baadhi yao kujiona bora kuliko wengine, hivyo kukatokea kudharauliana baina yao.

Pia kutoshirikishana kikamilifu kwa sekta binafsi na raia kwenye shughuli za ushirikiano na kutokuwapo kwa usawa katika kugawana matunda ya jumuiya baina ya nchi wanachama kwa wengine kuvutia kwao, hivyo wengine kufaidi zaidi na wengine kuhisi kupunjwa.

Hali hii ilisababishwa na tofauti ya viwango vya maendeleo baina ya nchi wanachama. Wakati Kenya iliendelea zaidi kiviwanda, Uganda na Tanzania ziligeuka kuwa soko kwa bidhaa za Kenya, hivyo kujikuta zinaifaidisha nchi moja na kujihisi kunyonywa!.

Kutokuwapo na sera maalum za kurekebisha tofauti hizi kulichangia, kwa kiasi kikubwa kuvunjika kwa jumuiya ya kwanza ya Afrika Mashariki.

Kutokana na kuvunjika kwa jumuiya hiyo mwaka 1977, nchi wanachama ziliajiri mpatanishi ambaye alihusika katika kugawa mali na madeni.

Kazi hii ilifanyika katika kipindi cha miaka saba yaani toka 1978 mpaka 1984, wakati nchi wanachama zilipotia saini makubaliano ya upatanishi yaliyotiwa saini Arusha, Tanzania Mei 24, 1984.

Miongoni mwa vipengele vya makubaliano ya upatanishi, kimojawapo kilikuwa kuangalia upya maeneo ambayo nchi za Afrika Mashariki zingeweza kushirikiana tena katika siku za baadaye. Imechukua zaidi ya miaka 10 kuamua maeneo mapya na kuunda taasisi nyingine ya ushirikiano.

Juhudi hizi zilianza na makubaliano ya Novemba 30, 1993 ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya Ushirikiano ili ihusike na uratibu wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiusalama na kisiasa. Makubaliano ya uanzishaji wa Sekretariati ya Tume ya Kudumu ya Ushirikiano yalitiwa saini Novemba 26, 1994.

Baada ya kutathmini hatua zilizochukuliwa na tume katika kuendeleza ushirikiano, viongozi wa Afrika Mashariki walifikia uamuzi huko Arusha, Tanzania, wa kuanzisha tena Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki, hivyo waliagiza tume kushughulikia majadiliano juu ya mkataba wa jumuiya hiyo mpya.

Matayarisho ya ufufuaji wa Jumuiya mpya yalikamilika mwaka 1999.

Mkataba wa Jumuiya Mpya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini na viongozi wa nchi za Afrika Mashariki, Arusha Novemba 30, 1999. Mkataba huu tayari umesharidhiwa na nchi zote wanachama na vyombo vyote muhimu vinavyotajwa katika Ibara ya 9 ya mkataba tayari vimeshaundwa.

### MTIKISIKO JUMUIYA YA PILI

Zile sababu zilizoifanya Jumuiya ya mwanzo kuvunjika, zilianza kujipenyeza tena kwenye jumuiya hii mpya kwa baadhi ya wanachama kutaka kuharakisha Mtangamano na kuvutia maslahi yao huku wengine wakisita, hivyo kukajitokeza vikundi vikundi na kujipachika majina kama kitu kilichoitwa 'The Coalition of the Willing" kumaanisha wale wanachama wenye haraka ya kuungana, wao waungane na kuwaacha wenzao ambao bado wanasita sita.

Kwenye jambo la pamoja, kunapojitokeza miamba miongoni mwao na kuanza kuonyeshana umwamba, kama kila mmoja atajifanya mwamba, ni lazima moto utawaka.

Lakini mmoja akijifanya mwamba mwingine ukijishusha, kunazuia moto kulipuka, hivyo The Coalition of the Willing ya miamba ilipoundwa, kuna wengine wakaamua kutumia busara kwa kujishusha kuipisha miamba badala ya kuonyeshana umwamba, hivyo kuikoa hii Jumuiya ya pili.

Tukutane Wiki Ijayo ambayo tutauchambua Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki sura kwa sura ili kuijua Jumuiya hii kwa karibu na vyombo vyake vikuu kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ambavyo ni Mkutano wa Wakuu wa Nchi; Baraza la Mawaziri wa nchi wanachama; Kamati ya Uratibu; Kamati za Kisekta; Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Bunge la Afrika Mashariki; na Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Daladala ya polisi inapokunywa mafuta ya umma!



Na Joseph Kulangwa

NYERERE! Namzungumzia Julius, mjukuu wa Burito! Mdogo wa Chifu Wanzagi! Baba wa Taifa la Tanzania. Mwalimu. Kama kuna vitabu alikuwa anavipenda maishani ni viwili; Biblia na Azimio la Arusha!

Alipata kukiri hivyo kwamba ndivyo alikuwa akitembea navyo. Kimoja cha ucha Mungu na kingine cha miiko ya utumishi na mapambano dhidi ya ukandamizaji, unyonyaji dhidi ya wanyonge.

Hakupenda sana kuzungumzia Biblia kwa sababu alijua kila mtu anajua, kwa nini ipo na ina dhima gani kwa maisha ya binadamu na uhusiano wake na Mungu wake wa mbinguni.

Alipenda kuzungumzia kile cha Azimio la Arusha, akikiita "kakitabu ka Azimio". Alikitumia kitabu hicho kuangalia maisha ya Watanzania yalivyokuwa yakienda na hasa akikumbuka jinsi Azimio la Arusha lilipotangazwa mwaka 1967 jijini Arusha.

Katika kitabu kile kilichokuja kusiginwa kwa kiasi na Azimio la Zanzibar katika miaka ya awali ya tisini, kulikuwa na miiko iliyozuia mtumishi wa umma kujilimbikizia mali na kutakiwa kujikita katika kutumikia wananchi.

Kwa kifupi kijitabu kile kilipinga ubepari, hivyo kiongozi wa umma ilikuwa marufuku kuwa bepari akitumia nafasi yake kujilimbikizia mali na kunyanyasa wanyonge waliotumikia Taifa kwa kuvuja jasho na damu.

Azimio la Zanzibar likaja kufungua milango kwa watumishi wa umma kujihusisha na biashara na kushindwa kujitofautisha na mabepari wengine waliopigwa vita na Azimio la Arusha.

Ilimuuma sana Mwalimu Nyerere alipoliona hilo na hasa aliposikia kumeingia Azimio la Zanzibar, lililokuwa kama vile linahalalisha kujilimbikizia mali na kuruhusu Ujamaa kuchechemea mbele ya Ubepari.

Sasa ikawa ruksa kwa mtumishi wa umma kumiliki mashamba makubwa, kumiliki maduka na biashara kubwa na mali zingine zilizompa utajiri na kujiwekea pengo kubwa kati yake na mlalahoi. Mwalimu ilimuuma lakini angefanyaje wakati hatamu alishaziachia, akabaki anasema na kunyamaza.

Ingekuwa enzi zile za utawala wa awamu ya tano, tungesema mstaafu huyo alikuwa anaweweseka kwani awamu yake ilishapita na sasa atuachie nchi yetu tuendeleze mapambano. "Wastaafu wapumzike, wanaweweseka, siku zao zimeshapita" (Kwa sauti ya kijana Ali Hapi akiwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa!).

Lakini Mwalimu alikuwa na sababu ya kusikitikia hali hiyo, kwa kutambua kuwa Watanzania wengi hawakuwa na hawako tayari hata sasa, kuishi maisha ya kibepari, kwani kufanya hivyo ni kutengana kitabaka kwa walionacho na wasionacho na siku zote wasionacho hupoteza.

Kuna nyakati nilipata kuandika kwenye safu ya gazeti moja hivi kuhusu baadhi ya watumishi wa iliyokuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (SUMATRA) na wa Jeshi la Polisi, kumiliki mabasi ya daladala na jinsi wanavyotumia fursa hiyo kujinufaisha.

Nilishambuliwa na aliyekuwa ofisa mwandamizi wa SUMATRA akitishia kunifikisha kwenye vyombo vya sheria nikathibitishe madai hayo, nikasimama imara nikimkaribisha milango ya Mahakama lakini akaufyata kwa sababu hata yeye alikuwa na daladala. Ila Mungu amlaze pema.

Watu hao walitumia nafasi zao kuhakikisha daladala zao zikifanya makosa ya usalama barabarani, basi zisichukuliwe hatua na hivyo kuonekana wako juu ya sheria kuliko wamiliki wengine wenye mabasi hayo wasio na nafasi serikalini.

Si hao tu, kuna viongozi wa serikali wanamiliki taasisi, shule na mambo mengine kama hayo na hata yanapofanya makosa yamekuwa yakitazamwa kwa macho ya upofu, huku wasio na nafasi hizo milki zao zikichukuliwa hatua za kufungwa au hata kufutwa.

Nilipomsikia Chifu Hangaya hivi karibuni akizungumzia suala askari Polisi kuwa na madaladala, lakini mbaya zaidi wakijichotea mafuta ya serikali na kunywesha madaladala yao kwa maslahi binafsi, sikushangaa, kwa sababu hilo lipo miaka mingi tu na linafahamika, lakini pengine mtafuna mfupa hakuwapo.

Mimi nimpongeze Chifu Hangaya kwa kulipata hilo na kuliweka hadharani, na kuonesha kuwa kumbe watu hawamsaidii kabisa, kwani ni jambo lililotakiwa kushughulikiwa huku chini na kumalizika bila hata kuhitaji hotuba ya Mkuu wa Nchi.

Pamoja na kwamba watu hawa hususan polisi wanatumia kofia zao kuchota mafuta ya Serikali kwenda kufanyia biashara, tunajua hawawezi kunyang'anywa madaladala yao kwa sababu wanaruhusiwa kuyamiliki lakini walioiba mafuta wabanwe. Kama alivyokataa Chifu Hangaya, polisi hawawezi kujichunguza, hivyo wachunguzwe hii ikome.

Watu waache pia kutumia nafasi zao za kikazi kufisidi mali za umma, huku wananchi wakiendelea kusota kwa ugumu wa maisha, wakichonganishwa na Rais wao mwenye nia njema ya kuwaondoa kwenye lindi la umasikini.

**Alamsiki!**

# Wamiliki majengo makubwa wapewa mbinu janga la moto

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Ulinzi na Usalama wa Hoteli ya Ramada mkoani Dar es Salaam, amewataka wamiliki wa majengo makubwa, zikiwamo hoteli, kutoa elimu ya janga la moto angalau mara tatu kwa mwaka kwa wafanyakazi na wateja wao ili tatizo linapojitokeza, wawe na utayari wa namna ya kujiokoa.

Fabiano Matawa alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam baada ya Hoteli ya Ramada Resort by Wyndham iliyoko Kunduchi, kuendesha tukio la dharura hotelini huko ambalo lilizua taharuki kwa wateja ambao kengele ya dharura ilipopigwa, walitoka ndani ya hoteli hiyo haraka wakidhani kuna tatizo.

Alisema wamekuwa wakifanya hivyo mara mbili kila mwaka bila kuwaeleza wateja ili kuona utayari wao pindi dharura inapotokea.

"Mfano likitokea janga la moto au lolote la dharura na hapa tupo karibu na Bahari ya Hindi, hatua gani za haraka za kuchukua? Kukumbushana ni kitu cha umuhimu kwa sababu tumekuwa tukishuhudia majanga ya moto kwenye majengo yakitokea," alisema.

Kiongozi huyo alisema wanapotoa elimu hiyo ya janga la moto kwa vitendo, halisaidii tu eneo la kazi, bali hata wanapokuwa majumbani pindi janga la moto linapotokea, mfanyakazi au mteja anajua mbinu za kujiokoa.

"Ninashauri hoteli zote Tanzania, kampuni na majengo makubwa, elimu ya janga la moto kwa vitendo ni kitu muhimu, ikiwezekana unaweza kufanya mara tatu kwa mwaka, lengo ni kuokoa maisha tukizingatia tupo ukanda wa Bahari ya Hindi inaweza kutokea janga lolote," alisema.

Mashaka Pesa kutoka Kampuni ya Ulinzi ya SGA, alisema wakiwa ofisini kwao, walipokea taarifa ya kuomba msaada wa dharura wa moto kutoka hotelini huko ndipo walipofika na magari maalum ya uokoaji.

"Tumekuja hapa kama tunakuja kuzima moto, hatukujua kama wanatoa elimu kwa watu wao, tumefika hapa tukakuta watu wote wameshatolewa, tukaingia ndani kuangalia, ndipo wakatuambia walikuwa wanatoa elimu," alisema. Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira na Usafi wa Hoteli ya Ramada, Robert Anthony, alisema wamekuwa wakifanya hivyo mara mbili kwa mwaka ili kujiandaa na janga la moto na dharura yoyote pindi zitapotokea.

Alisema hakuna madhara yaliyojitokeza wakati wakifanya dharura hiyo, akifafanua kuwa wageni ambao wako hotelini huko kutoka nchi mbalimbali, baada ya kusikia mlio wa dharura, walichukua tahadhari na kukimbilia eneo maalum lililotengwa bila kujali walikuwa wapi.

"Wateja wetu hatukuwaambia, lakini suala la dharura ni kitu ambacho wanakielewa kwenye nchi zao, walivyotoka nje ndipo tulipowataarifu kwamba tulikuwa tunafanya kama kukumbusha kuwa endapo tatizo likitokea hatua zipi wanapaswa kuchukua na hoteli inazichukua," alisema.

Mmoja wa wateja waliokuwapo hotelini hapo, Victor Sanga, alisema baada ya kusikia mlio wa dharura alipata mshtuko ndipo alipokimbilia nje kujua kilichotokea.

"Mpaka ninafika nje nilijua ni dharura, lakini tunashukuru watu wa dharura wa hapa na waliokuja wamekuwa wapesi, watu wanaohusika na huduma ya dharura wawe wanawahi kwenye matukio.

"Hatujui ni taarifa zinachelewa kufika kwenye uongozi, wawe wanafika kwa uharaka ili kuokoa maisha ya watu alafu vingine vifuate, pili elimu ya dharura iwe inatolewa mara kwa mara ili mtu awe anajua hatua ya kwanza iwe ipi," alisema.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2016/17, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alibainisha kuwa majengo mengi ya umma nchini si salama kutokana na kutokuwa na vifaa na mifumo ya kukabiliwa na majanga ya moto.




Wafanyakazi wa Hoteli ya Ramada Resort by Wyndham, wakiwa wamembeba majeruhi, wakati wa zoezi la kujipima utayari wa kukabiliana na majanga, lililofanyika hotelini hapo, Mtaa wa Kilongawima, Kata ya Kunduchi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## DC amulika ulinzi wa miradi ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka wananchi wa vijiji vya Mwandutu na Mwashagi wilayani Shinyanga kuitunza miundombinu ya miradi ya maji na kutoihujumu ili itumike kwa muda mrefu.

Aliagiza hayo juzi alipozuru na kukagua utekelezaji wa miradi ya maji kwenye vijiji hivyo ambayo inatekelezwa na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Shinyanga.

Yasinta aliwataka kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake na endapo wakiona mtu anataka kuharibu miundombinu hiyo ya maji, watoe taarifa kwa viongozi ili wamchukulie hatua haraka na kuzuia uharibifu huo.

"Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda sana wananchi wake na ndiyo maana amekuwa akitafuta fedha na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo hii ya maji na anatekeleza ilani ya CCM kwa vitendo.

"Ninawapongeza wananchi kwa kutoa maeneo yenu na kupitisha mabomba ya maji, huu ndiyo uzalendo tunaoutaka na muitunze miundombinu hii ya maji na kutoihujumu, atakayeiharibu tutamchukulia hatua kali," alionya.

Jasinta aliwataka wananchi wanapotaka kuunganishiwa maji majumbani mwao, wawatumie wataalamu na kuepuka vishoka.

Meneja RUWASA wilayani Shinyanga, Emmanuel Nkopi, alisema mradi wa maji katika Kijiji cha Mwandutu kwa kiwango kikubwa umekamilika na utaanza kutoa huduma ya maji ndani ya mwezi huu.

Alisema mradi wa maji katika Kijiji cha Mwashagi umekamilika na umeanza kutoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi.

Baadhi ya wananchi wa vijiji hivyo waliipongeza serikali kwa kutekeleza miradi hiyo ya maji iliyowaondolea shida ya kutumia maji machafu na kupoteza muda wa kufanya shughuli za maendeleo, wakitafuta maji vijiji jirani.

# Polisi watangaza kiama matumizi mabaya silaha

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limetangaza kuwapokonya bunduki watu wote wanaozimiliki kihalali lakini wanazitumia vibaya, ikiwamo kufanya uhalifu na mauaji.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alitangaza operesheni hiyo juzi ofisini kwake alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema kila mwaka jeshi hilo hufanya uhakiki wa silaha zote zinazomilikiwa kihalali na wanapobaini mmiliki wake amekiuka masharti, wanampokonya.

Alisema kuwa mbali na kuwapokonya silaha hizo, jeshi hilo pia linatoa mafunzo kwa wanaohitaji kununua silaha kwa mara ya kwanza ili kujua matumizi yake.

Akizungumzia matukio ya uhalifu mkoani kwake, Ng'anzi alisema kwa miezi minane ya mwanzo hakuna tukio la wizi wa kutumia silaha ambalo limeripotiwa kwao.

Alisema tayari wameshapokonya silaha mbalimbali zilizokuwa zikimilikiwa na watu kihalali baada ya kubaini kwamba wamiliki wake walikiuka masharti.

"Tayari tumepokonya silaha kutoka kwa baadhi ya watu waliokuwa wakizimiliki kihalali baada ya kubaini kuwa walizitumia vibaya ,ikiwamo kufanyia uhalifu pamoja na kufanya mauaji ya watu wengine," alisema

Akizungumzia operesheni maalum iliyotangazwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, ya kutaka watu wenye silaha haramu kuzisalimisha, Ng'anzi alisema mkoani kwake kazi hiyo imeanza.

Alisema kila mtu ambaye ana silaha aina ya bunduki ambayo haimiliki kihalali, aiwasilishe ofisi za vijiji, kata, wilayani au kituo chochote cha polisi kuanzia Septemba Mosi hadi 30 mwaka huu.

Alisema katika kipindi hicho mtu atakayefanya hivyo hatakamatwa wala kuchukuliwa hatua yoyote na baada ya muda huo kumalizika, polisi wataanza msako.

Ng'anzi alisema msako huo utakuwa mkali wa nyumba kwa nyumba, kijiji kwa kijiji na wilaya kwa wilaya ili kuhakikisha wanawanasa wote watakaokaidi agizo hilo.

"Waziri wa Mambo ya Ndani ametoa msamaha kwa watu wote wanaomiliki silaha isivyo halali kusalimisha silaha na sisi Jeshi la Polisi tunawaambia watu wote waziwasilishe katika maeneo hayo niliyoyataja na hawatachukuliwa hatua yoyote kati ya Septemba Mosi hadi 30 mwaka huu," alisema

Hivi karibuni serikali kupitia kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alitangazia watu wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria, kuzisalimisha bila kuchukuliwa hatua kati ya Septemba Mosi hadi 30 mwaka huu.

# MAISHA

SEPTEMBA 11, 2022
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Mayai hupunguza mwili



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jenga dari bora usijute baadaye




## KATUNIKA

Ukurasa 16


# USO UNAOVUTIA


## Huongeza utanashati kwa wanaume



Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | L | A | A | N | A |
| | A | | | Y | |
| M | W | A | | U | |
| | A | | I | N | A |
| | M | | | G | |
| S | A | U | M | U | |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ZOA, OTA, MAMBA, KAMBA, BOMOKA, KATAZA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

MSAIDIE TAU AFIKE NYUMBANI



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Alichokifanya Adaktari

MTOTO Jane alikuwa sebuleni na mama yake akijifunza kufuma kitambaa. Jane alitupia macho picha ya ukutani ambayo iliwaonyesha wavuvi wakivua baharini.

Baada ya kuona picha ile, Jane alikumbuka maneno ya mwalimu wake wa darasa.

Jane: Mama eti papa ndio samaki mkali baharini?

Mama Ndio mwanangu, tena wavuvi wanakuwa na tahadhari wanapokwenda kuvua baharini.

Jane: Mbona mwalimu ametuambia eti avumaye papa baharini lakini kuna wengine wapo.

Mama: Sawa lakini huo ni msemo tu unaosema unaweza kumdhania mabaya mtu, lakini kuna wengi wabaya zaidi yake.

Swali

Paa ni jamii ya Mnyama gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ahadi ya utajiri waganga wa jadi imenipa ufukara!

KARIBU tena msomaji wangu tumalizie sehemu ya mwisho ya kisa cha kijana Selestine aliyetamani kuwa tajiri kupitia waganga wa jadi. Alipitia masharti mengi mgumu hata hivyo ndoto yake ikazimika na kuwa fukara.

Msomaji wangu, kisa hiki nimekiandikia makala nne mfululizo na leo nakwenda kuhitimisha. Nikirejea kwa ufupi kwa faida ya waliopitwa na utangulizi wake, mganga aliyemfikisha kijana huyu hapo alipo, aliletwa nyumbani kwao mwaka 2011 na mume wa shangazi yake.

Na hiyo ni baada ya shangazi kujifungua boga badala ya mtoto. Na tukio hilo chanzo chake ni shangazi kumpokonya rafiki yake mume wake, hivyo rafiki huyo kumtamkia maneno mabaya. Ndipo shangazi akazaa boga hospitalini.

Mume huyo wa shangazi ndiye aliyemleta mganga huyo wa Burundi ategue kitendawili mkewe kuzaa boga. Mganga huyo kumaliza mazingaombwe yake na kurejea kwao, ndipo Selestine akaanza kusaka maisha.

Akauliza wenzake siri ya kufanikiwa, wakamwambia ni lazima aende kwa waganga apenye. Ndipo akamkumbuka yule mganga wa Burundi aliyekuja kwao shangazi alipojifungua boga.

Akamtafuta rafiki yake aitwaye Japhet waende Burundi kwa mganga ili kupata utajiri. Wakaondoka kwenda Burundi wakakuta amehamia Rwanda. Wakaelekezwa hadi kumpata.

Vijana hawa walipitia masharti magumu sana. Japhet alihudumiwa kwanza akapewa masharti ikiwa ni pamoja na kunywa maji yaliyooshea maiti na mengine kuyataja hapa ni vigumu. Masharti haya yalimshinda hivyo akashikiliwa mateka kusikojulikana.

Selestine naye alipewa masharti, yakiwemo kutafuta kamba aliyojinyongea mtu na kufa. Lingine gumu ni pale alipoingizwa ndani ya pango kwenye pori kubwa na kujikuta mbele ya joka kubwa la kutisha, lililojiviringisha mithili ya gurudumu kubwa la trekta.

Akatakiwa kusalimiana na joka hilo kwa kulambwa kiganja kwa ulimi wake, jambo ambalo alikataa. Akatozwa faini Sh.500 na kuzitoa papo hapo. Sharti lingine gumu ni pale alipoambiwa baada ya kurejea kwao anunue ndoo tatu azifunike zikiwa tupu na kuziweka ndani kwake.

Baada ya siku nne atafunua ndoo moja na atakuta shilingi milioni mbili. Hivyo akisikia mahali penye msiba jirani au mgonjwa au harusi, basi gharama zote atoe yeye kwa fedha hizo, jambo ambalo alilifanya ulipotokea msiba.

Katika huo msiba zilitakiwa Sh. 800,000 kwa ajili ya kusafirisha kwenda Tabora na pia gharama za chakula takriban Sh. 500,000 hivyo kufanya jumla Sh. milioni 1.3. Selestine alizitoa.

Akasema alipokwenda kufungua ndoo ya kwanza hakukuta tena fedha bali alikutana na kichwa cha mtu. Alipokiangalia vizuri kilionekana kama kimekaushwa au kibichi, yaani hakieleweki! Baada ya hapo akafungua ndoo ya pili akakuta nyoka mkubwa. Na alipofungua ndoo ya tatu akakuta kiganja cha mguu cha mtoto mchanga (unyayo).

Anasema, "baada ya hapo nikazifunika zile ndoo na kesho yake nikaenda kanisani kuonana na Padri. Naye akaniambia hapo ulipo una nguvu za kishetani (giza)". Akaniuliza; nyumbani una nini? Nikajibu sina kitu ila ndoo tatu. Akaniambia zina vitu ndani naviona, nenda kavichome au uvilete. Nami nikatekeleza maelekezo hayo.

Mpenzi msomaji, hayo ndiyo mapito ya Selestine kwa mujibu wa maelezo yake. Kwa sasa anaishi Mikumi mkoani Morogoro akibangaiza maisha. Kabla ya kwenda kwa waganga alikuwa na kazi ya kuchoma mkaa uliomwezesha kuishi na mkewe na mtoto.

Kwa mganga alitoa sh. 500,000 ili apate utajiri lakini ndoto ikayeyuka. Katikati ya simulizi yake, haraka nilimuungamisha sala ya toba ili Mungu amrehemu kwa kujiaminisha kwa waganga na kumsahau Mungu aliyemuumba mwenye utajiri wote.

Mpenzi msomaji, Mungu alituumbia kila kitu ndani yetu, lakini kwa kukosa kuwa na maarifa tukajiunganisha kwa mashetani tukapokwa vyote vizuri. Wengi huamini waganga wanaweza kuwatajirisha haraka, kumbe hilo ni chukizo mbele zake.

Ndiyo maana Mungu akaweka amri kuwa "Usiwe na miungu mingine ila mimi". Pia akasema: "Usivisujudie wala kuvitumikia kwa kuwa mimi BWANA, Mungu wako ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi na kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao."

Hivi sasa nimempa hela kidogo ya mtaji arudi kuchoma mkaa na Mungu atamuinua tena.

**Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Lazima tuyakabili mabadiliko ya tabianchi kuelekea COP27

MOJA ya matatizo makubwa yanayoikabili dunia na Tanzania ikiwamo ni kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha kutokuwapo mvua za kutosha, ukame, mafuriko na madhara mengine yanayotishia uhai wa watu.

Mabadiliko ya tabianchi hayasababishwi na eneo fulani pekee bali mchango wa dunia kwa ujumla, huku nchi za Afrika kwa ujumla wake zikichangia hewa ukaa chini ya asilimia nne na nchi zilizoendelea zikichangia kwa kiasi kikubwa.

Mathalani, kwa Tanzania mtu mmoja anachangai gesi ukaa kwa asilimia 0.22 kwa mwaka huku China na Marekani akichangia asilimia 26 kwa kipindi hicho hicho kutokana na shughuli za viwanda na zingine ndiyo maana nchi hizo zinatoa fedha za kusaidia kukabili mabadiliko ya tabianchi kwa nchi zilizotunza mazingira.

Hadi sasa hakuna mpango kwa nchi hizo kupunguza viwanda ndiyo kwanza vinaongezeka na ziko tayari kuendelea kutoa fedha kwa nchi zinazochangia kupunguza hewa ukaa kwa kutunza mazingira.

Kwa sasa kila eneo linakabiliwa na ukame huku maji ambayo ni muhimu kwa kila kiumbe yakiendelea kupungua. Migogoro baina ya binadamu na binadamu; wanyama na binadamu inaongezeka kwa sababu raslimali hiyo inapotea baadhi ya maeneo.

Ukisafiri kwa anga utaona hali ilivyo ardhini lakini kasi ya kupaa kwa bei ya nafaka kulikochagizwa na kupaa kwa bei ya mafuta ni udhihirisho kwamba ukame ni tishio. Pia unaona mito na maeneo mengine yalivyokauka.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilieleza mwelekeo wa mvua kuwa si wa kuridhisha. Wakulima wameshauriwa aina za mazao ya kulima ambayo ni ya muda mfupi na yenye kuhimili ukame.

Tunapoelekea kwenye mkutano wa wakuu wa nchi kuhusu mabadiliko ya tabia nchi COP27 utakaofanyika Cairo, Misri, ambao pamoja na mambo mengine kila nchi itaeleza ilivyotekeleza mpango wa kukabili mabadiliko hayo na afua zilizochukuliwa. Ni muhimu kujitathimini kama nchi namna ya kuhakikisha kila kiumbe hai kinaendelea kuishi kwa wakati huu.

Hadi sasa tunaona uhaba wa nafaka huku ikizidi kupanda bei, ongezeko la migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambao wanatoka maeneo yaliyohifadhiwa kwenda kutafuta malisho, huku binadamu nao wakivamia maeneo ya hifadhi kupata mahitaji ya Wanyama wafugwao.

Jitihada nyingi zimefanyika ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira, kupanda miti kwa wingi na kuachana na matumizi ya nishati ya kuni ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa mkaa unatumika zaidi kutokana na kupaa kwa bei ya gesi.

Hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu sana kwa sasa, nafaka zimepanda bei hali ya maisha inakuwa ngumu kutokana na visababishi vingine kama kupanda kwa bei ya mafuta na COVID-19.

Mabadiliko ya tabia nchi si jambo la kulichukulia rahisi, lazima nchi iendeleze mikakati yake ya kusaidia wananchi wake kuishi na hali hiyo ambayo haiwezi kuisha leo wala kesho kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Lazima jamii yetu iendelee kuelimishwa namna ya kutumia fursa katikati ya matatizo, mathalani kwa sasa kuna biashara ya hewa ukaa kwa wananchi waliotunza misitu ya asili, misitu ya kupanda na binafsi ambayo wanauza duniani kwa nchi zilizoharibu au zinazoharibu mazingira.

Misitu hiyo inasaidia kupunguza hewa ukaa kwenye anga na kukabili hali iliyopo sasa ya vipindi vya mvua kutoeleweka, ukame wa muda mrefu,joto na baridi kali kiasi cha kuathiri binadamu na viumbe wengine kama tunavyoona sasa maeneo mengi yana joto kali hadi misitu inawaka yenyewe na kwingine baridi sana.

Kwa sasa usalama wa chakula uko hatarini kwa kiasi kikubwa, kwamba wananchi hawana uhakika wa mlo kamili kutokana na kwamba hawana uhakika wa chakula chenyewe ili waendelee kuwa hai.

Kupambana na mabadiliko ya tabianchi ni lazima kwa kila mmoja lakini wananchi kutumia mbinu zao na za jumla kukabili hali hii,ili dunia iwe salama kwa kila mmoja anayestahili kuifurahia.

Kwa sasa tunasikia migogoro baina ya wanyama na binadamu inashamiri,wanyama wanatoka kwenye maeneo yao ya asili kutafuta malisho na binadamu anapeleka mifugo maeneo yaliyohifadhiwa kutafuta malisho,hii inafanya maisha yasiwe na amani kwenye maeneo mengi.

Mabadiliko ya tabianchi ni tishio lazima tuwe na mbinu zinazotekelezeka,kubuni namna ya kuendelea kupata maji ya mahitaji ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji kwa sababu cha mvua hakijaonyesha manufaa chanya.

Jitahada zinafanywa na serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali kama Chama Cha Waandishi wa Habari Tanzania (JET),chini ya mradi wa Tuhifadhi Maliasili wa USAID,ili kuelimisha jamii kutunza mazingira na hasa kuacha shughuli za kibinadamu kwenye mapito ya wanyamapori (shoroba) na mtawanyiko.







Jare Ijalana kutoka nchini Nigeria ndiye anayeelezwa kuwa mtoto mrembo zaidi duniani kiasi cha kupata nafasi ya kupamba majarida maarufu na kujiingizia pesa nyingi.







# MITINDO

## MALKIA ELIZABETH
### Mitindo ilikuwa maisha yake



MALKIA Elizabeth II amefariki dunia akiwa na miaka 96, huku akivunja rekodi ya kutawala nchi hiyo kwa miaka 70.

Kifo chake kimeleta simanzi duniani kote kutokana na kiongozi huyo kugusa kila Nyanja wakati wa uhai wake.

Katika tasnia ya mitindo, Malkia Elizabeth II, hakuwa nyuma kwani alihakikisha anavaa nguo za kisasa na zilizobuniwa na watu mashuhuri.

Mbunifu wake Fulton alikuwa akimtengenezea mavazi mengi ambayo yalileta gumzo kutokana na umaridadi wake.

Hata hivyo, Malkia mwenyewe alikuwa mpenzi wa mitindo, alipendelea kuona nguo yake , viatu, mkoba na mwamvuli vikiwa na rangi ya kufanana.

Kutokana na mapenzi yake katika mitindo, Malkia Elizabeth alipenda kuchagua rangi moja ya mavazi kila mwaka kwa ajili ya shughuli zake za kifalme.

Katika picha zake nyingi alionekana akiwa amevaa koti refu lililoambatana na gauni likiwa na rangi ya kung'aa kama kijani, njano, kijivu, nyekundu na bluu.

Katika tasnia ya mitindo unaweza kusema imempoteza mdau wake mkubwa na kwamba itachukua muda mrefu kumpata mtu mwingine kama yeye anayependa kuvaa mavazi ya kisasa.



## UREMBO
**Na Mary Geofrey**



# USO UNAOVUTIA
## Huongeza utanashati kwa wanaume

USO ni kitambulisho cha kwanza kabla ya kusikia sauti ya mtu akizungumza.

Haijalishi unafanya kazi kwenye mazingira gani, lakini cha kuzingatia ni unatunza vizuri ngozi yako ya uso ili kuboresha muonekano wake.

Mwanaume kuwa na ngozi nzuri huleta, furaha na kujiamini pia. Tumeona wanawake ndio wamekuwa mstari wa mbele kuboresha mwonekano wa nyuso zao, lakini kwa mwanaume ni muhimu pia.

Muonekano mzuri usoni ni mambo ambayo wanaume wanatakiwa kuyazingatia ni kama alama ya kujali ngozi na utanashati kwa jumla.

Kuna wanaume ambao hawana hata muda wa kujiangalia kwenye kioo labda kwa kudhani kuwa mambo hayo yanatakiwa kufanywa na wanawake jambo ambalo si kweli.

Kuna mambo mengi ambayo mwanaume anatakiwa kufanya ili aweze kuonekana na muonekano mzuri.

Miongoni mwa mambo hayo ni kuhakikisha unasafisha uso na kutakata, hapa unaweza kutumia taulo laini kwa kupaka kidogo sabuni na kisha safisha uso taratibu na baadaye unasuuza uso na kuufuta.

Unaweza pia kutumia Cleanser ambayo ni maalum kwa ajili ya kusafisha uso.

Si jambo la ajabu unapopita kwenye saluni na kukuta wanaume wakisafishwa uso au kufanya scrubing ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikisaidia kuondoa madoa usoni, mafuta na kufanya ngozi ipendeze.

Unaposafisha uso unaruhusu vitundu vya kutolea hewa kubaki wazi na hivyo kufanya ngozi kuwa na afya nzuri na hata muonekano wake kuwa bora zaidi.

Jitahidi kusafisha uso na kufanyia scrub uso wako japo angalau mara mbili kwa wiki itakusaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa seli zilizokufa kwenye ngozi.

Unaweza kuifanya ngozi yako ya uso kuwa laini na ya kuvutia.

Unaweza kupaka losheni au cream za kiume ambazo zipo madukani kwa ajili ya kuboresha zaidi ngozi yako.





## MAPISHI
**Na Mary Geofrey**

# Mayai hupunguza mwili

SOTE tunafahamu kuwa kuna ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayosababishwa na mtindo usiofaa wa maisha.

Moja ya sababu kubwa ni kula vyakula vyenye wanga ambavyo husababisha kuongezeka uzito na kusababisha baadhi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Katika kona yetu ya mapishi leo tutakumbushana vyakula vinavyofaa kwa ajili ya kutumia wewe mwenye nia ya kupunguza mwili wako.

Mayai

Watu wengi bado wanaamini kuwa mayai ni mabaya kwa afya hasa katika kuongeza cholesterol mwilini.

Ukweli ni kwamba kwanza kila kitu duniani kikitumiwa kwa wingi uliopitiliza huleta madhara fulani.

Mayai yapo katika orodha ya vyakula 10 bora duniani katika kusaidia kupunguza uzito kwa sababu yana kiasi kikubwa sana cha Protini.

Protini ndiyo fungu la chakula linaloongoza katika kupunguza uzito kwa sababu zifuatazo:

Protein hufanya ujisikie umeshiba kwa muda mrefu sana kwa sababu tumbo huhitaji muda mrefu zaidi kumeng'enya kundi hili la vyakula.

Kwa sababu protini hukaa tumboni muda mrefu hukusababisha kuondokana na ile hamu ya kula mara kwa mara.

Protini hutengeneza misuli ambayo ndiyo nyenzo kuu katika kuyeyusha mafuta mwilini.

Watu wengi wenye tabia za kula milo yenye protini nyingi hufahamika kuwa na afya nzuri na uzito unaotakiwa.

Mfano mzuri wa jamii ya watu wanaokula protini zaidi ni watu wa kabila la wamasai.

Jinsi ya kuandaa mayai

Unaweza kuchemsha au kukaanga mayai yako na mafuta kidogo ya nazi au ya Olive.

Ili ushibe vizuri zaidi unaweza kutengeneza omelette kubwa kwa kukaanga mayai pamoja na kuongeza mboga mboga unazozipenda kama pili pili hoho, uyoga, kabichi, vitunguu, mboga za majani kama spinach, nyanya, karoti.

Unaweza kula asubuhi na kikombe chako cha maziwa na ukashiba vyema hadi wakati wa mchana.

Wiki ijayo tutaendelea na vyakula vingine.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Jenga dari bora usijute baadaye

## Namna ya kusafisha feni za juu



NDANI ya nyumba ni muhimu kuweka kipoza joto juu ya dari.

Feni za juu zinaleta hewa nzuri, lakini zinapochafuka hewa huambatana na vumbi hivyo husababisha kero ndani ya nyumba.

Ili kupata upepo mwanana kila siku ni muhimu kufanya usafi kila wakati. Hizi ni baadhi ya dondoo za namna ya kusafisha pale unapoona uchafu.

1: Safisha mapanga yaliyo chini ya mota ya feni kwa uangalifu.

2: Tafuta kitambaa kikavu kidogo na ukikunje kwa ajili ya kufutia.

3: Unaweza kutumia sabuni ya kusafishia au ile ya kawaida ya kufulia.

4. Puliza dawa ya kusafishia kwenye ma panga na sehemu nyingine za feni na ufute taratibu na kitambaa.

5. Baada ya kumaliza kuisafisha subiri muda wa nusu saa kabla ya kuwasha.



KATIKA nyumba leo, tunazungumzia umuhimu wa kuzingatia umaliziaji mzuri wa dari kwenye nyumba.

Hii ni sehemu ambayo watu wengi wanaojenga nyumba, husahau kuipa kipaumbele Msanifu wa nyumba, Kimboi Marick, anasema hiyo ni sehemu muhimu zaidi kwa sababu ndio hupendezesha zaidi nyumba.

Marick anasema dari katika ujenzi wa nyumba mara nyingi watu wengi hawaipi uangalizi mkubwa, lakini ni sehemu muhimu isipomaliziwa vizuri inaweza kuharibu kabisa kazi yote nzuri ya ujenzi wa nyumba iliyofanyika.

Pia anasema kwa sababu inaficha vitu vingi kwa ndani, isipojengwa au kumaliziwa vizuri kitalaam inaweza kuleta athari kubwa kwenye nyumba.

"Dari imekuwa sehemu ambayo inasahaulika sana katika ujenzi wa nyumba zetu kwa maana ya kuwa inapewa uangalizi kidogo sana. Lakini umaliziaji mzuri wa dari hili ndio unaozidisha uzuri wa nyumba yako, inasaidia kuiweka imara na usalama zaidi" anasema Marick.


"Dari ndiyo inaficha mabomba ya umeme na huduma nyingine ikiwamo kuondoa uzia kwenye macho ya watu wanaoingia au kuishi kwenye nyumba husika na kuipa muonekano mzuri. Ili upate faida zote za dari hili ni vyema kumpata fundi au msanifu mzuri wa majengo anayeweza kusimamia kazi hiyo kwa ufanisi unaotakiwa," anaongeza.

Anasema kabla ya kufanya uamuzi wa umaliziaji wa nyumba yako ni vema ujitafakari na kufanya uamuzi kwanza wa aina ya muonekano wa dari unalolitaka kwenye nyumba yako ili kuepuka kujilaumu baadaye.

"Tafakari na uamue, unataka kupata mwonekano gani. Fanya uamuzi sahihi ni muundo gani wa dari unahitaji. Usikurupuke ili usije ukajilaumu baadaye, kumbuka kuna dari inayotakiwa kutengenezwa sebuleni, vyumbani, jikoni na hata vyooni. Na katika kila maeneo yote hayo unatakiwa kuamua.

"Unaweza kuamua muonekano wa dari la sebuleni ukawa tofauti na wa vyumbani au ukafanana, hiyo yote itategemea na namna unavyopendelea wewe, lakini la muhimu kuzingatia ni kwamba unatakiwa kuhakikisha unatumia watu ambao ni wataalamu ili wamalizie vizuri na kuiweka nyumba katika hali ya usalama zaidi," anasisitiza.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HII MIDENI YOTE YA MIFAINI MAKOSA UNAFANYA SAA NGAPI?
HATA NAJUA BASI?
KESHO NITAENDESHA MWENYEWE
DALA - DALA
WE BABA NANIHII EMBU RUDI NDANI TUELEWANE KWANZA
SITAKI! NA UKIZIDI KUNISUMBUA NAENDA JOBU HIVI HIVI
NIMESIKIA DODOSO ETI NA WEWE ULIKUWA KALANI WA SENSA?
HELA NILOLIPWA ISHEISHA!
KUFANYAKAZI HII NI BASI TU! LAKINI MIMI NI MSOMI
RISIKIRIZENI HIRI... KWANI MTU AKIWAONA MRIVYOURAMBIA ATABISHA KAMA NYIE HAMJASOMA WOTE?
LABDA KASOMA NA MJOMBA'AKE LAKINI SIO MIMI
KWANI KOSA LETU NINI MBONA TUPO MUNKIDE? TUPO CHELEA PINA
SHOSTI MUMEO KAJA KUNICHUMBIA JANA MCHANA KWEUPEEE LEO ANANIOA
NIMEMSIKIA INATAKIWA DAMU YA MKEWE WA NDOA SIJUI YA NINI? NJOO TUTAJUA
GHARAMA YA MAISHA
LIKIKUGANDA USILINUNIE LIZOEE ILI LIKUZOEE
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...BILA KUKATISHWA TAMAA HUFIKI UENDAKO...

# Charles III atangazwa rasmi kuwa mfalme wa Uingereza



Malkia Elizabeth akiwa na aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela.



Mfalme Charles III akiwa katika kiti cha enzi

**LONDON,** UINGEREZA

MWANAMFALME Charles III ametangazwa rasmi kama mfalme mpya wa Uingereza katika hafla ya kihistoria katika kasri la St James iliyofanyika jana asubuhi.

Bendera zilishushwa katika kumuombolezea Malkia, Elizabeth na ilipandishwa juu baada ya hafla hiyo kumalizika.

Hafla ya utanganzaji wa mfalme huyo mpya ilipeperushwa moja kwa moja kwenye televisheni kwa mara ya kwanza.

Charles alipokea Ufalme baada ya kifo cha mama yake Malkia Elizabeth II, aliyefariki jumamosi.

Baraza la kumtangaza rasmi Mfalme, lilijumuisha wanasiasa wakuu, majaji na maofisa wengine ambao walimtangaza rasmi kama mfalme.

Ni mara ya kwanza hafla hii inapeperushwa kwenye televisheni.

Matangazo mengine yatatolewa rasmi nchini kote Uingereza mpaka Jumapili, wakati bendera zitarudi kupepea nusu mlingoti.

Haya yanajiri baada ya Mfalme Charles kuahidi kumfuata, kipenzi mama yake kujitolea maisha kuhudumia watu katika hotuba yake ya kwanza iliyojaa huzuni.

Siku ya Ijumaa ameliambia taifa lake jinsi alivyohuzunika kwa kumpoteza mama yake, akisifia mzaha, ukarimu wake na uwezo wake wa kuona wema kwa kila mtu.

Mfalme ameahidi kulitumikia taifa kwa uwajibikaji usiotetereka kama aliokuwa nao marehemu mama yake Malkia katika utawala wake wa miaka 70.

Baada ya tangazo hilo, Mfalme atatoa tangazo binafsi kuhusu kifo cha Malkia na kula kiapo kulihifadhi kanisa la Uskotchi ambalo kuna mgawanyiko wa sheria kati ya kanisa na serikali.

Miongoni mwa watakaohudhuria hafla hii ni mkewe Camilla, ambaye amepokea wadhifa wa Malkia, mwanamfalme mpya wa Wales, William.

Tangazo la kwanza lilitolewa katika roshani ya Friar Court ya kasri la Mt. James mjini London saa tano saa za huko, muda unaoambatana na mbwembwe za wapiga tarumbeta, milio ya bunduki zinazofyatuliwa kwa heshima katika bustani ya Hyde na katika Jumba refu maarufu la London Tower.

Licha ya kwamba sio sehemu ya shughuli hiyo rasmi ya kutangazwa mfalme, maneno "Malkia amefariki, Mflame aishi Maisha marefu" mara nyingi hutamkwa baada ya hapo.

Juzi Charles alikutana na umati wa watu waliopiga kelele kumtakia maisha mema wakati akisalimiana na umati uliokuwepo nje ya kasri la Buckingham.

Baada ya hapo alitoa hotuba kwenye televisheni akieleza matumaini kwamba Mwanawe William kama Mwanamfalme mpya wa Wales na mkewe Catherine wataendelea kuwatia watu moyo na kuongoza mdahalo wa kitaifa.

**AFRIKA ITAMKUMBUKA MALKIA**

Malkia Elizabeth II alikuwa na nafasi maalum moyoni mwake kwa ajili ya Afrika, alikuwa barani humo katika nyakati muhimu za maisha yake.

Akiwa Afrika, wakati huo alikuwa akiishi katika Hoteli ambayo sasa imefungwa ya Treetops nchini Kenya, baba yake Mfalme George wa Sita, alipofariki na akawa Malkia akiwa na umri wa miaka 25 pekee.

Wakati wa utawala wake wa miaka 70 alitembelea zaidi ya nchi 20 za Kiafrika, na aliwahi kusema kwa mzaha mbele ya Nelson Mandela aliyekuwa akitabasamu kwamba amekuwa Afrika zaidi kuliko mtu yeyote, na kusababisha vicheko vikali kutoka kwa wale walio karibu naye.

Malkia huyo alikuwa na uhusiano mzuri binafsi na Mandela ambaye alikuwa rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini na kinara wa vita dhidi ya utawala wa wazungu wachache nchini humo.

Taasisi ya Mandela ilionyesha kusikitishwa kwake na kifo chake.

"Mandela na Elezabeth walizungumza kwenye simu mara kwa mara, wakitumia majina yao ya kwanza kama ishara ya kuheshimiana na vile vile upendo."

Taarifa hiyo ilisema alikuwa na jina maalum la Malkia, Motlalepula, ambalo linamaanisha Malkia wa mvua, kwa sababu ziara yake ya 1995 nchini humo wakati wa utawala wake iliambatana na mvua ya kumkaribisha.

Baada ya kurithi himaya kubwa iliyoenea katika bara la Afrika, baada ya kuwa Malkia enzi zake zilishuhudia makoloni yote 14 ya Waingereza katika Afrika yakipata uhuru wao, kuanzia na Ghana mnamo 1957.

Malkia aliweza kudumisha uhusiano wake na Afrika kwa kupitia uundaji wa Jumuiya ya Madola mwaka 1961, alipigwa picha akicheza na Kwame Nkrumah, ambaye aliongoza kampeni ya uhuru wa Ghana na kuwa rais wake wa kwanza.

Neno himaya liliachwa wakati wa kiapo chake cha kutawazwa mnamo 1953.

Viongozi kutoka barani kote Afrika wametoa salamu za pole kwa Uingereza

Rais wa nchi ya Kenya ambako safari yake kama Malkia ilianza, Uhuru Kenyatta, aliomboleza kifo chake akimtaja kama alama ya juu ya utumishi wa kujitolea kwa ubinadamu na kiongozi mkuu, sio tu Uingereza na Jumuiya ya Madola ambayo Kenya ni mwanachama mashuhuri lakini ulimwengu mzima.

Ingawa uhusiano kati ya Zimbabwe na Uingereza umekuwa sio mzuri kwa miaka mingi, jambo lililosababisha hayati Rais Robert Mugabe kujiondoa katika Jumuiya ya Madola, mrithi wake Emmerson Mnangagwa aliandika haraka kwenye Twitter kwamba anatoa pole ya dhati kwa Familia ya Kifalme na watu wa Uingereza, na Jumuiya ya Madola.

Kiongozi wa Nigeria, koloni kubwa zaidi la zamani la Uingereza barani Afrika, Muhammadu Buhari alimwandikia salamu za pole ndefu kwenye Twitter, akisema amepokea kifo chake kwa huzuni kubwa.

"Hadithi ya Nigeria ya sasa haitakamilika bila ukurasa wa Malkia Elizabeth ll, mtu mashuhuri duniani na kiongozi bora. Alijitolea maisha yake kufanya taifa lake, Jumuiya ya Madola na dunia nzima kuwa mahali pazuri."

Pia alimkaribisha mrithi wake Mfalme Charles III kwenye kiti cha enzi.

Rais Ali Bongo wa Gabon, ambalo ni koloni la zamani la Ufaransa ambalo lilijiunga na jumuiya hiyo mwezi Juni, pia ametuma salamu zake za rambirambi.

Licha ya kumiminika kwa salamu za rambirambi kutoka kwa viongozi wa bara hilo, baadhi ya Waafrika wengine wamezungumzia mateso yao chini ya utawala wa Waingereza, wakieleza kuwa ukoloni ulifanywa kwa jina la familia ya kifalme. Baadhi ya Falme zenyewe za Kiafrika pia wameelezea masikitiko yao.

Prince Mangosuthu Buthelezi alitoa heshima zake kwa niaba ya Mfalme Misuzulu KaZwelithini, kiongozi wa Wazulu wa Afrika Kusini.

Aliangazia urafiki wake wa kuthaminiwa na Mfalme Charles III, akimtumia salamu binafsi za rambirambi.

Mfalme Misuzulu yuko katika nafasi nzuri ya kuelewa kile ambacho Mfalme Charles anapitia, kwani baba yake mwenyewe, Zwelithini, alifariki mwaka jana, baada ya miaka 50 ya kiti cha enzi.

Malkia alikuwa kwenye ziara ya Afrika Kusini aliposherehekea siku yake ya kuzaliwa ya miaka 21 mwaka wa 1947.

Katika hotuba yake maarufu ya redio kutoka Cape Town, alijitolea maisha yake kwa Jumuiya ya Madola na kusema alijisikia nyumbani akiwa nchini Afrika Kusini kana kwamba alikuwa akiishi hapo maisha yake yote.

Akiwa maarufu duniani kote kwa uwezo wake wa kubaki kwenye siasa, alitoa kauli kali mwaka 1995, akizuru Afrika Kusini mwaka mmoja tu baada ya Mandela kuwa rais na kumaliza mfumo wa ubaguzi wa rangi uliohalalishwa unaojulikana kama ubaguzi wa rangi.

Aliipongeza nchi hiyo kwa maendeleo yake na kusema

"Mmekuwa taifa moja ambalo roho yake ya upatanisho ni mfano mzuri kwa ulimwengu, na nimerudi kujionea mwenyewe kile ambacho si muujiza mdogo."

**BBC**

## MAKALA

# SERIKALI YA WATU



Na Magabilo Masambu

JAMHURI ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo: Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii."

Hii ni kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi ibara ya 8(a). Duniani kuna aina nyingi za serikali. Ziko za kifalme, kijeshi na kadhalika. Zile zinazoitwa serikali za watu, maana yake zinapata madaraka kutoka kwa watu, kama ilivyo kwa serikali yetu. Tafsiri yake ni kwamba zinawekwa na watu kupitia sanduku la kura ili zifanye shughuli za kustawisha na kuboresha maisha ya watu.

Ikiwa wenye serikali kwa maana ya wananchi wanapiga kelele juu ya jambo fulani, wajibu wa serikali ni kusikiliza kelele hizo na ikiwezekana kuzitatua na kwa kufanya hivyo, inajiwekea dhamana ya kuendelea kukubalika na kuchaguliwa kila wakati. Kwa maana nyingine serikali wateja wake ni wananchi.

Ikiwa kuna mtu fulani anamiliki mgahawa wa chakula akatokea mteja akanunua chakula kile, wakati anakula akagundua kwamba kwenye chakula kile kuna mawe mengi, akapiga kelele kwa mmiliki wa mgahawa maana yake mtu huyo anapenda aendelee kuwa mteja wa mgahawa ule, ndiyo maana anasema kuna maweee.

Jukumu la mwenye mgahawa si kumwambia kama umeona kuna mawe usile au kale kwingine. Kama ni mwelewa kwanza, atamwomba radhi mteja wake ili asipoteze uteja huo. Pili ataahidi kurekebisha ili siku nyingine mteja wake huyo arudi tena.

Ukiwa na rafiki yako akaziona kasoro kwako, akakwambia usimchukie kwa sababu hatua ya kukwambia anahitaji kuendeleza urafiki na wewe vinginevyo alikuwa na uchaguzi wa kukaa kimya na kuvunja urafiki. Wapo wanaovunja urafiki kwa sababu ya kuambiwa ukweli, maana ni watu wachache sana duniani wanaovumilia kuambiwa ukweli na kuukubali kisha kuchukua hatua ya kufanya marekebisho.

Siku hizi ukiingia kwenye mabasi, utaona pembeni ya kuta za basi kuna vimatangazo kwa abiria, kwamba dereva akizidisha mwendo piga simu namba hizi. Kwa hiyo abiria wana haki ya msingi kabisa kupiga kelele kwenye basi wanapoona dereva amezidisha mwendo na kupiga kelele huko ni kulinda maisha yao binafsi na ya dereva vile vile, kwa sababu gari likipata ajali yeyote anaweza kupoteza maisha.

Ukimchapa mtoto haki alio nayo ni kulia. Inawezekana kilio chake kitakufanya unayemtandika umwonee huruma, lakini ikiwa utamtandika mtoto halafu asilie wala kutoa chozi. Maana yake mtandikaji anaweza kuchukulia kwamba mtoto yule anacho kiburi cha kutosha, hivyo fimbo zitaongezeka japo imetokea mara nyingi mtu anatandika mtoto huku akimwambia nyamaza! Ukitaka anyamaze ni kuacha kipigo lakini huwezi kuendelea kutandika huku ukitaka anyamaze, hiyo ni kumnyima haki yake ya kulia.

Ikiwa kijiji fulani hakuna maji wananchi wanalia kazi ya serikali ya watu si kuwaambia kaeni kimya huku wakiwa hawana maji, watakaa kimya kwa kuwekewa maji safi na salama. Vivyo hivyo, kwenye huduma zingine kama barabara, dawa hospitalini na shule.

Tunatambua serikali haiwezi kutuliza vilio vya wananchi bila kutoa huduma zinazotakiwa na kutoa huduma hizo inahitaji ushirikiano wa wananchi katika kutekeleza mipango yake kama inavyotamkwa na Katiba ya nchi yetu ibara ya 8(d) inayosema; "Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii."

Kushiriki huko lazima kuwe na makubaliano kati ya wananchi na serikali yao. Kushiriki lazima iendane na ushirikishwaji maana yake wananchi na serikali kwa maana ya viongozi wao wakubaliane kwenye mambo kadhaa ili kujiletea maendeleo kwa pamoja.

Mfano, viongozi wanaweza kuwaeleza wananchi kwamba ili kutekeleza shughuli zetu za maendeleo kama serikali, tumeona tupunguze matumizi ya serikali kwa kutotembelea magari ya bei kubwa na ninyi wananchi changieni hiki ili tufanikishe maendeleo yetu maana ni yetu sote. Barabara zikijengwa si za wananchi tu wala viongozi tu bali wote tutapita, wananchi wanaona naam kama viongozi wamefanya hivyo sisi tutafanya zaidi.

Sasa hivi kuna malalamiko ya tozo kila kona. Yaani unakwenda benki unatoa pesa ili uweke kwenye simu unakatwa, unaweka kwenye simu unatuma unakatwa, anayepokea anakatwa. Huu ni ulipaji wa kodi wa namna gani? Kuna haja ya serikali kusikiliza kelele hizi za wananchi kwa sababu wanaopiga kelele wanaitakia mema serikali wala hawawezi kuwa maadui.

Ushauri wangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuwa katiba imekupa mamlaka ya kuwa msemaji wa mwisho ni vema kuingilia kati jambo hili. Kelele kazi yake huwa ni kuonyesha kwamba kuna tatizo, bora watu wapige kelele kwa sababu zitakusaidia kutambua wapi kuna tatizo wapi hakuna. Tukijenga utamaduni wa kunyamazisha watu, hatutajua wapi tunapatia wapi tunakosea.

Ni kweli kwamba tozo hizi zinajenga miradi ya maendeleo lakini kama zimekuwa kero ni muda sasa wa kuwaita wachumi wa nchi hii kina Prof.Lipumba, Dk. Kaaya wa pale Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) na wengine ambao wako nje ya serikali washirikiane na walioko serikalini kuainisha ni vyanzo gani vya mapato, vinaweza kutumika mbadala wa tozo ili kupunguza kelele za wananchi ambao nia yao ni njema kabisa.

Waziri wa fedha huko mitandaoni amekuwa anasakamwa sana. Jambo hili sasa limebadilika na kuwa kama lake binafsi. Mtu huyu ana familia na ndugu, wanajisikiaje kuona anasemwa vibaya maana lolote analolifanya kwa sasa inaonekana ni pesa yetu ya tozo.

Nadhani si jambo jema sana pamoja na kwamba yeye ndo msimamizi wa masuala haya, kuna haja ya kurudi nyuma na kutazama tena hata kama ni sheria za bunge. Imani yangu ni kwamba kikao cha bunge kinachotarajiwa kuanza keshokutwa kitafanyia kazi malalamiko haya ya wananchi na kuondoa mtazamo mbaya juu ya waziri wa fedha kwa kuondoa tozo na kutafuta mbadala wake.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Maquiz, Bima Lee wanavyofichua uongo kutumika kwenye mapenzi*



Na Adam Fungamwango

INAELEZWA eti tangu enzi za mababu kuwa mwanamume akimpenda mwanamke uongo ni lazima utumike japo kidogo. Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema kama 'hukumpiga kamba' mwanamke huwezi kumpata. Unachotakiwa ni kudanganya kidogo tu kwa ajili ya kushawishi kama vile mwanasiasa anavyoomba kura. Wakati mwingine kile anachoahidi kwa wapigakura wake hawezi kukitekeleza.

Kwanza kabisa, ieleweke kuwa uongo ni dhambi. Binadamu hatakiwi kusema uongo kwa njia yoyote ile. Unaweza kuongea uongo duniani ukafanikiwa kupata unachokihitaji, iwe mpenzi, mke au mali lakini ni vya hapa duniani. Mbele ya safari ni hasara kubwa.

Lakini pia kwa uchunguzi wangu mdogo, nimegundua kuwa uongo kwa wanaume kuwadanganya wanawake kwa lengo la kuwashawishi wawakubali, unaanzia miaka ambayo binadamu waliashaanza kutawanyika kwenda kutafuta maisha sehemu zingine na si zile karne za watu wanaozaliwa hapo hapo kijijini na kufia hapo bila kufika hata makao makuu ya mkoa.

Waliokuwa wakiishi enzi hizo ilikuwa huwezi kumdanganya mwanamke kwa sababu ni mtoto wa hapo hapo kijijini, amezaliwa hapo na kukulia hapo. Mwanamume huyo hawezi kufanya hivyo kwa sababu kila mtu anakuwa anajulikana yeye, wazazi hadi ukoo na watu wote kijijini hapo.

Hiyo ilitumika hata kwa wanaume kupata wake bora. Kwa sababu wanafahamiana, wazazi wanamwambia mtoto wao wa kiume aoe ukoo fulani na ukoo mwingine asioe.

Ataambiwa matatizo yao na kwenye sifa ataambiwa. Hata kwa msichana, mvulana ataambiwa tabia za mwanamke anayemtaka kama ni mzuri amuoe, au mbaya aachane naye.

Dunia ya sasa ya utandawazi, kuna changamoto kubwa kwenye ndoa kwa sababu hakuna anayemfahamu mwenzake vyema. Kila mtu anaficha 'makucha' au tabia mbaya aliyo nayo isionekane mapema kwa mwenzake.

Tabia zinaanza kuonekana ndani ya ndoa. Kila mmoja anashindwa kuvumilia tabia asizozijua kwa mwenzake na ndoa inaanza kuyumba na kuanguka.

Kuna uongo fulani unaofanana na ukweli unaweza kuutumia kwa msichana ili kuweka mazingira mazuri, lakini mwingine baadaye unamdhalilisha hata aliyeutumia.

Unaweza labda ukamwambia msichana nina nyumba ili akukubali, lakini kumbe nyumba ni ya familia au ya urithi au ya kupanga.

Unaweza kumwambia msichana kama una kazi kumbe ni kibarua tu. Kwa sababu unapata pesa na unamudu maisha, basi ataamini kuwa una kazi ya kuajiriwa.

Tatizo ni pale unadanganya kuwa wewe ni mkurugenzi au meneja, wakati hata kazi yenyewe au kibarua tu huna, hili ni tatizo kubwa.

Bendi kadhaa ziliwaona watu wa aina hiyo na kutunga nyimbo ambazo ziliwaonya na kuwatahadharisha mabinti kuwa makini.

Tunaanza na Pendo wa Bima Lee Orchestra. Unaanza kwa mwanamume kulalamika kwa uchungu kuondoka kwa mpenzi wake Pendo na roho imenyong'onyea. Binti hataki kuvaa mitumba na kumwambia mpenzi wake heshima itashuka.

"Pendo mimi mumeo kazi yangu ni kibarua wa kuponda kokota hapa mjini masikini eee, aaa Pendo. Elimu ya ngumbaru, kisomo cha mwembeni, kisomo changu cha ukubwani, pesa nitazipata wapi? "

Mwanaume analalamika juu ya kuondoka mpenzi wake, akimueleza ukweli kuwa maisha na elimu yake ni duni. Hapa hivyo ni kweli alimwambia hivyo mapema wakati anamtongoza?

"Usiniambie chochote mume wangu, ulipokuja kwetu kunioa ulikuja na gari la fahari na kusema wewe ni mhasibu mjini. Tena una miradi ya kufuga kuku na nguruwe, itakuwaje leo uniambie ni mponda kokoto?"

Mke anakumbuka alivyoingizwa 'mkenge' mwanzoni lakini alipofika mjini akakuta ni tofauti, hivyo akakasirika.

"Sura yako nzuri na umbile lako zuri ndilo lililosababisha nikudanganye, lakini mpenzi ukumbuke tangu zamani mwanamume akimpenda mwanamke, uongo ni lazima usemwe japo kidogo." Hapo mume anajitetea.

Huu nao ni uongo wa kiwango cha lami. Unafanana kabisa na ule wa 'Karubandika' wa Maquiz Original.

"Kama wewe ungenipenda, kwa nini kunidangaya bwana we, kujibandika madaraka siyo yako bwana wewe. Nimesikia tetesi kuwa huna lolote hata kazi huna eee. Unazurura mchana kutwa kupita kurandaranda mitaani, kumbe hukuwa na uwezo wa kunioa ila kuniharibia maisha, heri kunieleza ukweli kuliko kunidanganya, nikuelewe vipi, babu ee uaminifu wako uko wapi ee, bwana.

"Usinione bwege baba, kwa kukubali wito wako Karubandika, hayo yote ni matatizo ya dunia baba. Nilitaka kujitumbukiza ndani ya moto, kumbe bwana yule hana kitanda wala shuka, pa kulala hana analala kwenye stendi ya basi, na kituo cha Uda.

Akiingia kwenye baa kazi yake kuomba bia, hana hata aibu sigara pia aomba, mitaani na kwenya mastoo hujitangazia kuwa yeye ni Mkurugenzi wa Kampuni fulani, kumbe sivyo hivyo."

Dada huyu amemnanga vilivyo Karubandika. Halafu kwa bahati nzuri alishtuka mapema, angeolewa huyu, sijui ingekuwaje! Kwa wanaume wote, uongo kama huu ni hatari si kwa wasichana wanaowaongepea, lakini kwao pia.

**Tuma meseji 0716 350534.**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-18

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

BASI niwaambie tu, mtoto mwenyewe niliyemlea nikiwa mdada wa kazi ni wewe Prince.”

Mshtuko uliotokea hapo kati ya Prince na Hasnat ulikuwa mkubwa. Pamoja na kuifuatilia hadithi yote hiyo, lakini hawakutegemea kama mwisho wake utakuwa huo.

“Ina maana...” Akauliza Prince kwa kigugumizi akiwa amehamanika.

“Ina maana kuwa Martin na Hilda ndiyo wazazi wako halisi. Martin ndiyo baba yako mzazi na Hilda ni mama yako mzazi.”

Kabla hajaendelea kuhoji zaidi, Prince alionekana kushindwa kujizuia, akaanza kulia.

Ilikuwa ni kazi ya Hidaya na binti yake kumbembeleza.

“Pole mwanangu, hii ndiyo dunia, ina makubwa. Wa kale walisema dunia ni tambara bovu. Lakini ashukuriwe Mungu amekuongoza kufika kwa mama yako mdogo. Yote ni mipango ya Mungu.

Nadhani sasa umepata jibu kwa nini nilikuwa nakuita mwanangu tangu mwanzo kabisa nilipotambua.” Hidaya alikuwa anaongea maneno haya huku akimbembeleza Prince ambaye wakati huo sasa alikuwa sasa amenyamaza kulia kwa sauti.

Bado alikuwa akilia kimoyomoyo. Kwa mara ya kwanza sasa ndiyo anatambua baba na mama yake mzazi ni nani. Moyoni bado alikuwa na maswali tele.


“Pole Prince, nyamaza mwaya.” Ilikuwa sauti laini ya Hasnat iliyoonekana kubembeleza vema huku akimshika mkono kitu ambacho kilimfariji.

Awali wakati Hidaya alipoanza kusema ni mama yake, mawazo ya kuwa na uhusiano na Hasnat yalianza kumuondoka tangu alipoanza kumwambia yeye ni mama yake.

Na alipoanza kuelezea alihofia isije ikamalizikia kuwa Hidaya ni mama yake mzazi ikawa sasa badala ya kuwa mpenzi, akageuka kuwa dada.

Ni kweli hadithi ya Martin na Hilda haikumalizikia alikodhani, lakini ilimuuma alipoambiwa ndiyo wazazi wake.

Faraja kidogo aliyoipata ni kwamba hakuwa ndugu wa damu na Hasnat, kwa hiyo hadhani kama kuna kipingamizi kitakachomzuia kumpenda.




**“Sikiliza mwanangu, huyo mzee baada ya mama yako kujiua, alinitimua kazi, ukabaki kwake na mimi nikaanzisha maisha yangu ambayo ndiyo haya unayoyaona.**

“Mama mdogo ulinitambua kwa sababu ya makovu ya mkononi na mdomoni, je niliungua wapi na ilikuwaje?” Lilikuwa swali la kwanza aliloliza kwa sauti ya chini na upole akionekana kabisa ameumizwa na kisa hicho kilichofanya kujua ukweli wa wazazi wake halisi.

Hidaya hakutegemea tena swali hilo, lakini akalijibu.

“Uliungua kwenu kwa baba yako Martin na mama yako Hilda, mimi niliinjika sufuria la uji kwenye jiko la mchina, nikatoka nje kuanua nepi zako kufika tu, na wewe ukawa umefika jikoni, kabla sijaongea chochote, ukawa umepeleka mkono kwenye sufuria, likaanguka, uji ukakumwagikia mkononi, hapo pembeni mwa mgongo na kifuani.

Bahati nzuri kwa sababu mimi niliiona lile tukio linafanyika haraka haraka nikakimbia kukuokoa. Kama ningekuwa nje, sijui saa hizi tungekuwa tunaongea hadithi gani.

Kwa bahati nzuri ambayo hadi leo nawakumbuka baba na mama yako, hawakunifukuza, kunifokea, wala kuniona mzembe, walichukulia ni bahati mbaya, tukakupeleka hospitali ukapona nikaendelea.

Ndiyo maana hata baba yako alipofariki mama yako alinichukua kwenda kwa mzee Simon.”

“Huyu mzee Simon ndiyo nani?” Hili ndiyo swali ambalo Hidaya alitegemea kuulizwa mwanzo.

“Kwani huyo anayejiita baba yako mzazi anaitwa nani?” Hilda naye akauliza swali badala ya kujibu.

“Mzee Pokwa.”

“Hujui lingine?”

“Ndiyo.”

“Basi huyo anaitwa Simon Pokwa. Huyo mzee anayejifanya baba yako mzazi ndiye aliyemuua baba yako halisi kwa kutuma wauaji wa kukodi waliomuua na maiti kuiweka kwenye gari lake wakaitupa kwenye korongo, na pia alimtishia kumuua mama yako kama atatoroka kwake, ikasababisha mama yako akajiua.”

“Mama mdogo, kwa nini anafanya yote haya? Baada ya kuwaua wazazi wangu akanichukua mimi na kuanza kunifundisha silaha, akanilea kipweke sana, akanidanganya yeye ndiyo baba yangu mzazi, akanijaza hasira na uongo kuwa kuna watu walimuua mama yangu mzazi kwa ugomvi wa shamba na yeye mwenyewe akawa ananituma niwateketeze?”

“Sikiliza mwanangu, huyo mzee baada ya mama yako kujiua, alinitimua kazi, ukabaki kwake na mimi nikaanzisha maisha yangu ambayo ndiyo haya unayoyaona.

Na sikuwahi kukutia tena machoni hadi nilipokutambua kwa hayo makovu.”

“Sasa na hawa ambao alikuwa ananituma niwaue ukiwemo wewe?”

“Mwanangu ni kwamba kama nilivyokwambia, baba yako alikuwa na mali nyingi kama mzee Simon.

Alikuchukua na kukulea mwenyewe ili kudhulumu mali na biashara za baba yako. Pili alijua ukichukuliwa na ndugu wa wazazi wako ambao walipambana sana bila mafanikio, wanaweza kupata nguvu ya kisheria kwa sababu marehemu alikuacha bado mdogo kwa hiyo mali zitaenda kwako licha ya kwamba ni mdogo, lakini ndugu itabidi wazisimamie. Hilo hakulitaka kabisa. Akahonga akashinda kesi.

Alihofu pia ukiwa mkubwa unaweza kulipiza kisasi, ndiyo maana alikuchukua na kukupandikiza mbegu mbaya.

Akakulea kwa tahadhari na upweke usionane na watu ambao wangeweza kukunong'oneza ukweli kama huu ninaokuambia kabla hajatimiza azma yake.

Ukaanza kuua watu ambao ndiyo muhimu kwako.

Na sasa ndiyo nimefahamu kwa nini huyo mzee amekutuma uniue na mimi. Ili tu usijue ukweli halisi kuhusu wazazi wako.”

“Na wale wengine niliowaua walikuwa ni akina nani? Na kwa nini alitaka wau wawe?”

“Nassor na Hassan wale ni mawakili ambao walikuwa na nyaraka zote za mali za baba yako. Walisubiri mtoto wake awe mkubwa na kufungua kesi.

Sabri anafahamu kisa chote cha baba yako kuuawa na kutupwa kwenye korongo, alikuwa shahidi mzuri sana kwako, Hussein ni mjomba wa mama yako, kabla ya kujiua aliandika barua ya kwa nini anafanya hivyo, na akataka kama mtoto wake mdogo anayemuacha duniani akiwa mkubwa amkabidhi.

Yaani alikuwa na barua yako akukabidhi ili ujue ukweli.

Alimpigia simu akamwambia mjomba wake afike nyumbani mara moja na chini ya meza kuna barua ataikuta.

Alifika na kukuta amejiua, lakini akaipata hiyo barua. Miaka ilivyozidi kwenda mzee Pokwa aligundua hilo, akawa anamuwinda kumuua ili kuzia kitu chochote kisijulikane. Wewe pia ukahusika kufanya mauaji.”

ITAENDELEA JUMAPILI



# THE WARRIORS VOICES SASA 'WAOMBA' KWA MUNGU

KUNDI linalofanya muziki wa injili, The Warriors Voices, wameibuka kivingine na video ya wimbo mpya, 'Omba' ambayo imeanza kufanya vizuri kwa mashabiki.

Akizungumza na BT jana, mwalimu wa kundi hilo, Adam Mniko, amesema ni muda wa kuikumbusha jamii kuomba na kuzungumza na Mungu kila wakati kwa njia ya maombi.

"The Warriors Voices tunamtukuza Mungu kwa kuendelea kututumia, safari hii tumekuja na wimbo unaitwa Omba ambao tayari upo kwenye mitandao yote ya kijamii hasa channeli yetu ya YouTube hivyo tunaomba sapoti ili huduma yetu izidi kuchanua," amesema Mniko.

# RUGA, NYANSHISKI KUWASHA MOTO DAR



KWA mara ya kwanza uongozi wa EAST Africa Redio na Televisheni kwa kushirikiana na waandaaji wa matamasha ya burudani ya muziki The Works, watawashusha nchini mastaa wa muziki kutoka Nigeria kutoa burudani ya kufa mtu.

Katika Shoo hiyo itakayofanyika Oktoba mosi, mwaka huu Ruga kutoka Nigeria na Nyanshiski wa Kenya wataungana na mwanamuziki nyota wa kizazi kipya kutoka hapa nchini Jay Melodi, kuwasha moto jukwaani.

Katika uzinduzi wa kampeni ya tamasha hilo uliofanyika katika ofisi za EAST Africa Redio na Televisheni Mikocheni Dar es Salaam, Mkurugenzi wa tamasha hilo kutoka The Works, Ahmed Ali, aliwahakikishia mashabiki kuwa shoo hiyo itakuwa na mambo mengi ya kuvutia ambayo hayajawahi kutokea.

"Kila kitu katika tamasha hili kitakuwa kikifanyika kwa mara ya kwanza, kuna mambo mengi yameandaliwa ambayo ninauhakika watanzania watayafurahia kwani kutakuwa na ubunifu wa hali ya juu katika eneo litakapofanyika tamasha pamoja na burudani isiyokifani itakayotolewa na wasanii mbalimbali," alisema Ali.

Aliweka wazi kuwa katika tamasha hilo kutakuwa na tiketi za aina tatu ya VVIP, VIP na kawaida, na gharama zitakuwa kuanzia 40,000 hadi 80,000.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SON :SINA WASIWASI NA MWANZO MBAYA

## Ana matumaini mambo yatabadilika na ataanza kung'ara katika...

**LONDON,** England

SON Heung-min ameapa atakuwa mchezaji bora licha ya kuanza kwa mwenendo mbaya msimu huu.

Tottenham Hotspur wameanza msimu bila kupoteza, na majuzi waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Marseille 2-0 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mshambuliaji huyo nyota bado hajafunga bao katika mechi saba.

Kocha, Antonio Conte ameendelea kumwamini mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini katika kikosi chake cha kwanza na Son mwenyewe amedai anaamini mambo yatakuwa bora.

"Hii itanifanya kuwa na nguvu zaidi. Hili ni jambo ninaloona litakuwa na maendeleo kwa sababu bado nina nafasi kubwa ya kujiboresha," alisema Son akinukuliwa na BT Sport.

**"Kama timu na kama mtu bin afsi pia, muhimu zaidi ni kwamba tunafanya hivyo.**

"Kiukweli kama ningekuwa sipati nafasi kwenye mchezo ningekuwa na wasiwasi.

"Lakini bado napata nafasi, katika baadhi ya michezo kumekuwa na matukio ya bahati mbaya, katika baadhi ya michezo kumekuwa na umaliziaji mbaya.

"Katika baadhi ya michezo huwa nachanganyikiwa kwa sababu nikipata nafasi kubwa na mpira usiingie ndani, inanifanya nicheke tu.

"Lakini sina wasiwasi nayo kwa sababu timu na wachezaji wenzangu wanafanya vizuri.

"Nadhani nikifunga moja kujiamini kutakuwapo tena na natumaini naweza kuendelea na kufunga mabao zaidi."

## KWA UFUPI

### ALLISTER ATAJWA ARSENAL

EMMANUEL Petit ameishauri klabu yake ya zamani ya Arsenal kumsajili kiungo wa Brighton na Argentina, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 23, wakati wa dirisha la usajili la Januari. (***Mirror***)

### GVARDIOL AMVUTIA POTTER

KOCHA, Graham Potter anamwania mlinzi wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 20, akitaka kuufanya usajili wake wa kwanza kama kocha wa Chelsea. ***(Express)***

### KARIUS SAFI NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imekubali kumsajili golikipa wa zamani wa Liverpool, Loris Karius mwenye umri wa miaka 29. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani yupo huru baada ya kuondoka Liverpool. (***Football Insider***)

### GRIMALDO AINGIA SOKONI

NEWCASTLE inapanga kuingia katika mbio moja na Arsenal kuwania saini ya mlinzi wa kushoto wa Benfica na Hispania, Alex Grimaldo, mwenye umri wa miaka 26, ambaye yupo kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba na anaweza kupatikana kwa pauni milioni 8.6. (***Mirror***)

### SANTOS KUTUA NEWCASTLE

KIUNGO wa Vasco de Gama na Timu ya Taifa ya Brazil, Andrey Santos mwenye umri wa miaka 18 pia anawaniwa na Newcastle United. (***iNews***)

### MUDRYK AITAKA ARSENAL

WINGA wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21, amesema hataweza kusema "hapana" kwa Arsenal kama klabu hiyo itataka kumsajili kutoka Shakhtar Donetsk. (Sun)

### NAPOLI YAMKATAA RONALDO

KLABU ya Napoli haikuwa na mpango wa kumsajili fowadi wa Ureno na Manchester United, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo. (***Mirror***)

### DALOT APIGANIA NAMBA

MLINZI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, amesema alikataa ofa ya kuhamia AC Milan ili kupigania nafasi yake pale Old Trafford. (***Metro***)

### ARIAS : NINAIWAZA UNITED

MLINZI wa kulia wa Colombia ambaye ni mchezaji huru kwa sasa, Santiago Arias, mwenye umri wa miaka 30, yupo tayari kujiunga na Manchester United baada ya kuondoka Atletico Madrid kipindi cha majira ya joto. (***Mirror***)

### 'KUONDOKA HAALAND KICHEKO'

MKURUGENZI wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl, amesema alikuwa na furaha kumuuza mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland kwa Manchester City kipindi hiki cha majira ya joto, kwa sababu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 angekuwa mzigo kwa klabu hiyo. (***Sport Bild, via 90min)***

### ALBA KUIBEBA BARCELONA

MLINZI wa kushoto wa Hispania, Jordi Alba mwenye umri wa miaka 33, amejipanga kuendelea kuichezea Barcelona, licha ya kuhusishwa na Inter Milan kipindi cha majira ya joto. (***Marca***)

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,029,4

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
MALLORCA
1 | 1.26
X | 5.85
2 | 9.49

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HATIMA YA LUKAKU INTER KIZUNGUMKUTI



**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku atajadili mustakabali wake na Inter Milan baada ya Thomas Tuchel kutimuliwa katika klabu ya Chelsea.

Fowadi huyo wa Ubelgiji alikosa nafasi chini ya Mjerumani huyo katika msimu wake aliorejea Stamford Bridge na akajiunga tena na Inter Milan kwa mkopo wa msimu mzima.


Lakini kwa sababu sasa Tuchel hayupo katika klabu hiyo na kuwasili kwa Graham Potter kutaamua mustakabali wa Lukaku.

Chelsea iliziba pengo la kuondoka kwa Lukaku kwa mkopo kwa kumsajili Pierre-Emerick Aubameyang kutoka Barcelona, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon akiwa amewahi kufanya kazi na Tuchel katika klabu ya Borussia Dortmund siku za nyuma.

Akizungumza na Sky Sports Italia, Mkurugenzi Mtendaji wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, alikiri klabu haina uhakika kitakachofuata baada ya mabadiliko ya wasimamizi: "Ni habari mpya. Sijui madhara ya mabadiliko ya kocha yatakuwaje.

"Tunataka kupata kiwango bora zaidi kutoka kwa Lukaku, na kisha mwisho wa msimu tutakaa na kuzungumza juu yake na Chelsea.

"Sijui kama mabadiliko ya kocha yanamaanisha kurudi kwake ni moja kwa moja, ni vigumu kutabiri leo."



# Torres awacheka wanaomdhihaki

**BARCELONA,** Hispania

FERRAN Torres amecheka na uvumi kuhusu uwezekano wa yeye kuondoka Barcelona.

Fowadi huyo alijiunga na timu hiyo ya LaLiga Januari mwaka huu na alikuwa mchezaji muhimu kwa upande wa kocha Xavi katika kipindi cha pili cha msimu uliopita.

Hata hivyo, tangu wakati huo amepoteza nafasi yake katika kikosi cha kwanza cha wachezaji 10 baada ya kuwasili kwa Robert Lewandowski na Raphinha katika dirisha la usajili la majira ya joto.

Huku Ousmane Dembele akivutia na Ansu Fati yuko sawa tena, inaonekana nafasi ya kucheza zitakuwa chache kwa Mhispania huyo.

Kuelekea mwisho wa dirisha la usajili, ilisemekana Arsenal walikuwa wanataka kutumia fursa hiyo kumleta Emirates, lakini jambo hilo halikufanyika na imeripotiwa watajaribu kumsajili ifikapo Januari.

Hata hivyo, amecheka mazungumzo kama hayo, akisema hana mpango wa kuondoka hivi karibuni baada ya kujiunga na anafurahia kuongezeka kwa ushindani wa nafasi.

"Njia ya kutoka? Sasa hivi nimefika Barca!" alisema akinukuliwa na AS.

"Ni fahari kwamba mchezaji kama huyu (Lewandowski) yuko hapa, tayari tunamfahamu na tunajua yeye ni mchezaji wa aina gani. Kumekuwa na wachezaji wengine waliosajiliwa, tunapambana kutengeneza timu yenye ushindani, ambayo ndiyo Barca wanastahili."

401,974/-

# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs Nice | 3.13 | 3.03 | 2.38 |
| 02. 11/09/22 | 16:00 | Angers vs Montpellier | 2.42 | 3.46 | 2.72 |
| 03. 11/09/22 | 16:00 | Toulouse vs Reims | 2.22 | 3.41 | 3.07 |
| 04. 11/09/22 | 16:00 | Bologna vs Fiorentina | 2.90 | 3.35 | 2.38 |
| 05. 11/09/22 | 16:00 | Lecce vs AC Monza Brianz | 2.24 | 3.34 | 3.14 |
| 06. 11/09/22 | 16:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.64 | 3.43 | 2.54 |
| 07. 11/09/22 | 16:00 | Ilves Tampere vs Inter Turku | 2.83 | 3.33 | 2.43 |
| 08. 11/09/22 | 16:00 | Honka vs HJK Helsinki | 2.69 | 3.24 | 2.59 |
| 09. 11/09/22 | 16:30 | FC Koln vs Union Berlin | 2.38 | 3.31 | 2.87 |
| 10. 11/09/22 | 17:00 | Cercle Brugge vs Royal Antwerp | 2.84 | 3.44 | 2.37 |
| 11. 11/09/22 | 19:00 | Aalesunds vs Sarpsborg | 2.35 | 3.48 | 2.84 |
| 12. 11/09/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Viking | 2.98 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 11/09/22 | 20:00 | CS Maritimo vs Gil Vicente | 2.78 | 3.13 | 2.59 |
| 14. 11/09/22 | 20:00 | FC Arouca vs Boavista | 2.63 | 3.08 | 2.78 |
| 15. 11/09/22 | 20:00 | Kayserispor vs Antalyaspor | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 16. 11/09/22 | 21:45 | Monaco vs Lyon | 2.46 | 3.46 | 2.67 |
| 17. 11/09/22 | 22:00 | Betis vs Villarreal | 2.79 | 3.38 | 2.44 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 11/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 2234 | Utrecht vs Vitesse Arnhem | 1.88 | 3.65 | 3.65 |
| 13:30 | 2491 | Atalanta vs Cremonese | 1.31 | 5.19 | 8.18 |
| 14:00 | 5972 | Strasbourg vs Clermont Foot | 1.64 | 3.77 | 5.02 |
| 14:30 | 5080 | KVC Westerlo vs Anderlecht | 2.77 | 3.37 | 2.40 |
| 15:00 | 2831 | Real Madrid vs Mallorca | 1.26 | 5.85 | 9.48 |
| 15:00 | 2905 | Nordsjalland vs Midtjylland | 2.70 | 3.46 | 2.40 |
| 15:00 | 5473 | Fakel vs Lokomotiv Moscow | 2.94 | 3.39 | 2.24 |
| 15:15 | 4569 | Servette Geneva vs FC Zurich | 1.95 | 3.66 | 3.46 |
| 15:30 | 1354 | Cambuur vs Groningen | 2.12 | 3.50 | 3.10 |
| 15:30 | 2036 | Austria Lustenau vs LASK Linz | 4.44 | 3.95 | 1.61 |
| 15:30 | 3719 | TSV Hartberg vs Austria Vienna | 3.00 | 3.34 | 2.14 |
| 16:00 | 1593 | Toulouse vs Reims | 2.22 | 3.42 | 3.01 |
| 16:00 | 2180 | AC Ajaccio vs Nice | 3.11 | 3.01 | 2.37 |
| 16:00 | 2648 | Sassuolo vs Udinese | 2.60 | 3.40 | 2.49 |
| 16:00 | 3293 | Marumo Gallants FC vs Kaizer Chiefs | 3.90 | 2.90 | 2.09 |
| 16:00 | 3466 | Lorient vs Nantes | 2.09 | 3.21 | 3.51 |
| 16:00 | 4175 | Lecce vs Monza | 2.22 | 3.26 | 3.11 |
| 16:00 | 4617 | Bologna vs Fiorentina | 2.85 | 3.30 | 2.34 |
| 16:00 | 4771 | Angers vs Montpellier | 2.40 | 3.46 | 2.70 |
| 16:30 | 5707 | FC Koln vs Union Berlin | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 17:00 | 1346 | Sivasspor vs Istanbulspor | 1.80 | 3.56 | 4.21 |
| 17:00 | 3169 | Dynamo Kiev vs FK Lviv | 1.17 | 6.28 | 11.78 |
| 17:00 | 3507 | Cercle Brugge vs Royal Antwerp | 2.81 | 3.41 | 2.35 |
| 17:00 | 5283 | Brondby vs Randers | 2.05 | 3.46 | 3.36 |
| 17:15 | 3174 | Elche vs Athletic Bilbao | 3.94 | 3.39 | 1.92 |
| 17:30 | 2001 | BSC Young Boys vs FC Lugano | 1.42 | 4.74 | 6.25 |
| 17:30 | 2064 | Pacos Ferreira vs Casa Pia Atletico | 2.77 | 3.02 | 2.62 |
| 17:30 | 2949 | Zenit St Petersburg vs Gazovik Orenburg | 1.12 | 7.62 | 17.05 |
| 17:30 | 4933 | FC Basel vs Grasshoppers | 1.59 | 4.03 | 5.04 |
| 17:45 | 4546 | AZ Alkmaar vs Twente | 2.09 | 3.35 | 3.30 |
| 18:05 | 4471 | Rennes vs AJ Auxerre | 1.40 | 4.72 | 6.62 |
| 18:30 | 2917 | Malmo vs Norrkoping | 1.54 | 4.03 | 4.91 |
| 18:30 | 4380 | Olympiakos vs Volos | 1.25 | 5.44 | 11.08 |
| 18:30 | 5282 | SC Freiburg vs Monchengladbach | 1.99 | 3.60 | 3.35 |
| 19:00 | 5094 | Lazio vs Verona | 1.56 | 4.09 | 5.19 |
| 19:30 | 2053 | Getafe vs Real Sociedad | 3.59 | 2.98 | 2.19 |
| 19:30 | 4674 | Union Saint Gilloise vs Racing Genk | 2.07 | 3.51 | 3.26 |
| 19:45 | 1580 | Rostov vs Spartak Moscow | 2.84 | 3.44 | 2.28 |
| 20:00 | 2515 | Kayserispor vs Antalyaspor | 2.56 | 3.31 | 2.61 |
| 20:00 | 2582 | Kasimpasa vs Galatasaray | 3.88 | 3.73 | 1.82 |
| 20:00 | 2882 | FC Arouca vs Boavista | 2.60 | 3.05 | 2.75 |
| 20:00 | 3850 | Gaziantep BB vs Umraniyespor | 1.73 | 3.68 | 4.43 |
| 20:00 | 3955 | Maritimo vs Gil Vicente | 2.76 | 3.11 | 2.56 |
| 21:00 | 3021 | Feyenoord vs Sparta Rotterdam | 1.26 | 5.62 | 9.03 |
| 21:30 | 5265 | Panathinaikos vs AEK Athens | 2.24 | 3.11 | 3.26 |
| 21:45 | 4082 | Juventus vs Salernitana | 1.44 | 4.21 | 6.74 |
| 21:45 | 4687 | Monaco vs Lyon | 2.45 | 3.45 | 2.65 |
| 22:00 | 1796 | KAA Gent vs Zulte Waregem | 1.34 | 5.04 | 7.66 |
| 22:00 | 4899 | Betis vs Villarreal | 2.78 | 3.34 | 2.44 |
| 22:30 | 2512 | Rio Ave vs Sporting Braga | 5.03 | 3.92 | 1.61 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# POLISI, CHIPUKIZI KIBARUANI LIGI KUU ZANZIBAR IKIREJEA

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MZUNGUKO wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar unatarajiwa kuendelea tena leo katika viwanja nane ambapo Polisi Zanzibar itaikaribisha Chipukizi kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Finya ulioko Pemba.

Timu zote mbili zitashuka dimbani zikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi zao zilizopita.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itawakutanisha Uhamiaji dhidi ya Jamhuri wakati Dulla Boys ambayo ilianza msimu kwa ushindi itaivaa Taifa Jang'ombe iliyovuna pointi moja katika mchezo wake wa kwanza walipokutana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Polisi Zanzibar, Ali Mtuli, alisema mchezo wake dhidi ya Chipukizi utakuwa mgumu na wenye ushindani hivyo amejipanga kupambana kuondoka na pointi tatu.

Mtuli alisema wanaingia uwanjani wakiwa na uchungu wa kupoteza mechi za kwanza hivyo anahitaji kuona anaanza vyema mzunguko wa pili.

Kocha huyo alisema kwa upande wake amekiandaa vyema kikosi chake kwa kurekebisha makosa mbalimbali aliyoyaona katika mchezo wa kwanza ili yasijirudie.

"Tumejipanga imara na tumedhamiria kuondoka na alama tatu muhimu, lakini kwa sababu tutakuwa ugenini, ninahitaji kucheza kwa tahadhari na umakini mkubwa," alisema Mtuli.

Aliongeza kila timu inapocheza katika uwanja wake wa nyumbani inahitaji kuhakikisha haipotezi mchezo na kwa maana hiyo amewataka wachezaji wake watambue wanakutana na wapinzani wa aina gani.

"Tunaenda kucheza ugenini tena Kisiwani Pemba, lazima mpinzani wetu awe amejipanga kuhakikisha anautumia vyema uwanja wake wa nyumbani baada ya kupoteza mchezo wake wa kwanza wa msimu tena alikuwa nyumbani, timu zote zitacheza kwa tahadhari na hofu ya kufungwa baada ya kupoteza mchezo wa awali, nasisi tumejipanga," alisema kocha huyo.

Hata hivyo Mtuli alisema licha ya mchezo huo kutarajiwa kuwa mgumu, anaamini kikosi chake kitaondoka na alama zote tatu za ugenini.

KMKM ambao leo wanakabiliwa na mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly Tripoli kutoka Libya ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar.



Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camilius Wambura (kulia), akizungumza na wachezaji wa timu mbalimbali za jeshi hilo wanaoshiriki Mashindano ya Majeshi ya Ukanda wa Kusini mwa Afrika yanayoendelea kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Biashara kuanza na Fountain

**Na Adam Fungamwango**

BIASHARA United iliyoshuka daraja msimu uliomalizika, itaanza kampeni ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwavaa Fountain Gate FC katika mechi itakayochezwa Septemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Gairo, mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), hiyo itakuwa ni moja ya mechi ya kuanza kwa Ligi ya Championship itakayotimua vumbi kwenye viwanja mbalimbali nchini.

Mechi nyingine zitakazochezwa siku hiyo itakuwa ni kati ya Gwambina dhidi ya Mbeya Kwanza wakati Mashujaa FC watakuwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma wakiwakaribisha Transit Camp, Kitayosce watacheza dhidi ya African, huku African Sports wakiwavaa Green Warriors.

Kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha wenyeji Mbuni FC watawaalika Ndanda FC, JKT Tanzania itakuwa nyumbani wake kwenye Uwanja wa Meja Isamuhyo kupambana na Copca FC la Pamba wataipokea KenGold ya Mbeya.

Bingwa na mshindi wa pili wa ligi hiyo watapanda daraja moja kwa moja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa mwaka 2023/24.

# Michezo

Jumapili Septemba 11, 2022
Nipashe



Son :Sina wasiwasi na mwanzo mbaya HABARI UK 21



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Zalan FC katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Geita Gold FC dimbani Sudan

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara, Geita Gold FC wanatarajia kushuka ugenini kuwavaa Hilal Alsahil katika mechi ya hatua ya awali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo jijini Khartoum, Sudan.

Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Minziro aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na wamejipanga kuanza vyema michuano hiyo ya kimataifa.

"Wachezaji wangu wana morali kubwa, wameahidi watatimiza kile tulichokifanya mazoezini, tumejiandaa kupata ushindi ili kuianza vizuri safari yetu," alisema Minziro.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Geita Gold, Simon Shija, alisema kila kitu kinakwenda vizuri na kilichobakia ni kusubiri muda wa mechi.

"Tumekuja Sudan kupambana, tunahitaji kuweka rekodi nzuri katika mashindano haya, tunaamini tutafikia malengo," Shija alisema.

Wakati huo huo, Kipanga FC ya Zanzibar inatarajia kushuka ugenini kuwavaa Hial FC ya Sudan Kusini katika mchezo wa hatua ya awali wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# Simba SC, Yanga zatakata

### ●●● Mayele apiga hat-trick ya kwanza, Bocco akizindukia Malawi ambapo...

**Na Waandishi Wetu**

MAMBO safi, ni baada ya wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba kupata ushindi wa mabao 2-0 ugenini Malawi wakati Yanga iliwachapa wenyeji, Zalan FC magoli 4-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ilikuwa ni siku nzuri kwa mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, ambaye alifunga hat- trick katika mchezo huo, lakini ikiwa ni mara yake ya kwanza kuondoka na mpira tangu alipojiunga na klabu hiyo mwaka jana.

Mayele alifunga bao la kwanza dakika ya 46 ya kipindi cha pili, bao la tatu dakika ya 85 na dakika ya 89 akimalizia msumari wa mwisho kwa kuunganisha krosi iliyopigwa na Mkongomani mwenzake, Djuma Shabani.

Kiungo Mtanzania, Feisal Salum 'Fei Toto' aliifungia timu hiyo bao la pili dakika ya 55 baada ya kupokea pasi kutoka kwa Mayele ambaye tayari alikuwa ameshawanyanyua mashabiki wa Yanga ambao walijitokeza kushuhudia mechi hiyo.

Hata hivyo, timu hizo zilimaliza dakika 45 za kipindi cha kwanza zikiwa suluhu licha ya Yanga kutawala mchezo huo kwa kutengeneza nafasi nyingi za wazi ambazo hazikutumiwa vyema na washambuliaji wake.

Pia golikipa wa Zalan FC, Major Majok, alionekana kikwazo kwa Yanga kupata mabao katika kipindi cha kwanza kutokana na kuokoa mashambulizi mbalimbali yaliyoelekea kwenye lango lake hadi mambo yalivyomzidia kwenye dakika 45 za mwisho.

Mabao ya Mzambia Moses Phiri na nahodha, John Bocco yaliiwezesha Simba kuondoka na ushindi wa ugenini wa mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets na kuiweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Ikiwa kwenye Uwanja wa Bingu Mutharika, Lilongwe nchini Malawi, Simba ilicheza tofauti na ilivyokuwa katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Jumatano iliyopita dhidi ya KMC ambayo ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Nyota ilianza kumwakia Phiri tangu dakika ya pili alipomchungulia kipa, Richard Chimbamba, akiwa ametoka golini, akapiga shuti la juu mita takribani 35, lakini bahati nzuri kipa alirudi nyuma haraka na kuuwahi mpira.

Nyasa Big Bullets ingeweza kupata bao dakika ya 21 baada ya Gomezgani Chirwa kupiga faulo iliyomkuta Adepoju Batatunde ambaye akiwa kwenye msitu wa mabeki wa Simba aligeuka na kupiga shuti, lakini ulimbabatiza Mohamed Outtara kabla ya Henock Inonga kuufagia hatarini.

Dakika ya 29, Phiri aliiandikia Simba bao la kwanza kwa staili ya 'tiktak', akiunganisha mpira wa faulo iliyopigwa na Clatous Chama.

Faulo hiyo iliyopigwa ilipita kwenye msitu wa wachezaji wa Simba na Nyasa Big Bullets na kumkuta mfungaji aliyelipa goli la wapinzani mgongo, ghafla akajikunja na kuupiga mpira ambao ulijaa wavuni, akimwacha Chimbamba akiwa amesimama tu.

Baada ya bao hilo, wenyeji walihaha kutaka kupata bao la kurudisha, na dakika 30, Chimwemwe Idana, aliwalamba chenga mabeki wa Simba na kuachia shuti kali lililodakwa vyema na Tanzania One, Aishi Manula.

Beki Outtara, nusura alizawadie Nyasa Big Bullets bao dakika ya 40, alipoanguka mwenyewe katika harakati za kumpiga chenga Kerstein Simbi, ambaye aliuchukua mpira akiwa kwenye wingi ya kulia na kupiga krosi ya hatari, lakini Manula akikaa imara na kuudaka.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, Simba ikiwatoa Kibu Denis, Sadio Kanoute, Phiri na Pape Sakho, nafasi zao zikachukuliwa na Augustine Okra, Peter Banda, Erasto Nyoni na Bocco.

Hata hivyo ni kipindi ambacho kilitawaliwa zaidi na Nyasa Big Bullets ambao walifanya mashabulizi mengi mfululizo na kuliweka rehani lango la Simba.

Dakika saba kabla ya mechi kumalizika, Simba ilipachika bao la pili kupitia kwa Bocco aliyemalizia kazi nzuri iliyofanywa na Chama.

Katika hatua nyingine, mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wameshindwa kuutumua vyema uwanja wa nyumbani kwa kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Al Ahly Tripoli ya Libya.

Mabao ya Al Ahly Tripoli katika mchezo huo uliochezwa kwenye Uwanja wa Amaan yalipachikwa na Ayed Ayoub dakika ya 41 na Imhammed Abdallah aliyefunga dakika ya 62.

Yanga itarudiana na Zalan ifikapo Septemba 17, mwaka huu ambapo KMKM itakuwa ugenini mjini Bangal kuwavaa Al Ahly Tripoli na siku inayofuata Simba itawaalika Nyasa Big Bullets kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Imeandaliwa na Saada Akida, Adam Fungamwango (Dar es Salaam) na Hawa Abdallah, Zanzibar.**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >